# CHUO KIKUU CHA NAIROBI

**FANI KATIKA *UTENZI WA MWANA HASINA NA RASHID WALII***

**AGNES WAITHIRA MUCHIRI**

**Tasnifu Hii Imetolewa Ili Kutosheleza Baadhi Ya Mahitaji Ya Shahada Ya Uzamili Katika Chuo Kikuu Cha Nairobi.**

**AGOSTI, 2016**

## UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na wala haijatolewa katika chuo kingine chochote nchini Kenya.

Agnes Waithira Muchiri

____________________ ____________________

Sahihi Tarehe

NAMBARI YA USAJILI C50/67162/2013

Tasnifu hii imewasilishwa kwa madhumuni ya kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimamizi walioteuliwa na Chuo Kikuu cha Nairobi

____________________ ____________________

Sahihi Tarehe

Prof. Kineene Wa Mutiso

(Msimamizi)

____________________ ____________________

Sahihi Tarehe

Dkt. Nyachae Michira

(Msimamizi)

## TABARUKU

Tasnifu hii ninaitabarukia wazazi wangu wapendwa Charles Muchiri na Ann Muchiri kwa kunipa elimu. Mume wangu mpendwa Zachary Theuri kwa kunisaidia kwa hali na mali wakati nilipokuwa nikisoma. Aidha, kwa kunipa moyo wa kuendelea na kazi yangu ya utafiti pamoja na kunipa utulivu wa moyo na akili. Hatimaye, watoto wangu wa dhati Bridgit na Joy, kwa kunivumilia kwani niliwanyima mahitaji muhimu nikimakinika katika masomo yangu.

**SHUKRANI**

Kazi hii imekuwa na panda shuka nyingi lakini kwa usaidizi wa watu mbalimbali nimeweza kukamilisha. Kwanza, namshukuru mwenyezi Mungu aishiye milele kwa kunipa afya njema na akili timamu pamoja na hekima ili kufanikisha malengo yangu ya kiusomi. Ni kupitia kwa nguvu na uwezo wake ambapo nimeweza kutimiza ndoto yangu ya kupata shahada ya uzamili katika somo la Kiswahili.

Shukrani za dhati nazitoa kwa wasimamizi wangu Prof. Kineene Wamutiso na Dkt. Nyachae Michira kwa kunielekeza na zaidi ya hayo kunivumilia. Aidha, ni kupitia kwa juhudi zao ambapo kazi yangu imeweza kukamilika kwa wakati ufaao na kuwa ya kutamanika. Fauka ya hayo, shukrani za pekee zimwendee Prof. Kineene Wamutiso kwa kunipa *Utenzi wa Mwana Hasina na Rashidi Walii*, kama si yeye singeupata.

Shukrani zingine ziwaendee wahadhiri wangu wapenzi walionifunza: Prof. Kineene Wamutiso, Prof. John Habwe, Prof. Mwenda Mbatiah, Dkt. Iribe Mwangi, Dkt. Evans Mbuthia, Dkt. Prisca Jerono na Dkt. Zaja Omboga. Vilevile wahadhiri wengine wa Chuo Kikuu cha Nairobi ambao walinifunza na kunisaidia kwa njia moja au nyingine Mungu awabariki nyote na awape hekima na siku nyingi muwasaidie wengine kama mimi.

Pia, ninawashukuru wasomi wengine tulioshirikiana nao, kushauriana pamoja na kuhimizana. Wao ni: Bosibori, Njeri, Jacquline, Faith, Kimeto, Simon, Agnes, Winfred, Adelin na Asha miongoni mwa wengine. Asante kwa ushirikiano wenu.

Hatimaye, ningependa kutoa shukrani za kipekee kwa sahibu wangu wa karibu sana Florence kwa kunielekeza na kunipa ushauri. Pamoja na hayo, kunipa msaada wa kila aina niliouhitaji. Mungu akubariki sana na akupe hekima zaidi. Zaidi ya hayo, namshukuru Mumbi kwa kujitolea kunipigia chapa kazi zangu zote za kiusomi pamoja na kuzipanga na kuyarekebisha makosa yaliyojitokeza.

Kwenu nyote ambao sikuwataja kwa majina na mlinifaa kwa njia moja au nyingine, nawashukuru sana na Mungu awabariki.

# IKISIRI

Utafiti huu ulilenga kuhakiki kipengele cha fani katika *Utenzi wa Mwana Hasina na Rashidi Walii*, ulioandikwa na Saidi Abdullah Masud (1964) na kuhaririwa na Knappert (1967). Mada hii ilichaguliwa kwa misingi kwamba, kipengele hiki cha fani hakijawahi shughulikiwa katika utenzi huu. Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya Urasimu wa Kirusi, kwa vile ilionekana kufaa zaidi kubainisha kipengele hiki cha fani. Aidha, utafiti huu ulifanywa maktabani. Data iliwasilishwa kwa njia ya maelezo. Madhumuni ya utafiti huu yalikuwa kubainisha vipengele mbalimbali vya fani, vilivyotumika Katika *Utenzi wa Mwana Hasina na Rashidi Walii* na pia kutathmini mchango wake katika kuwasilisha maana ya utendi unaohusika. Malengo yanayorejelewa yalitumiwa kuundia nadharia tete zilizoongoza kubainisha vipengele vya fani na mchango wake katika utenzi ulioteuliwa. Aidha, utafiti wetu umebainisha kuwa vipengele vya fani ndivyo nguzo kuu iliyotumika katika kuwasilisha ujumbe. Vipengele vya fani ambavyo ni nguzo kuu ni kama vile: Msuko, muundo, mandhari wahusika na uhusika na matumizi ya lugha. Matokeo ya utafiti huu ni kuwa mtunzi ametumia vipengele vya fani kama vile: Msuko, muundo, wahusika na uhusika na matumizi ya lugha kwa njia iliyofaa ilikuwasilisha ujumbe wake.

## YALIYOMO


UNGAMO ........ ii

TABARUKU ........ iii

SHUKRANI ........ iv

IKISIRI ........ v

**SURA YA KWANZA ........ 1**

1.1 Utangulizi ........ 1

1.2 Tatizo la utafiti ........ 2

1.3 Madhumuni ya utafiti ........ 3

1.4 Nadharia tete ........ 3

1.5 Sababu za kuchagua mada hii ........ 3

1.6 Upeo na mipaka ........ 4

1.7 Yaliyoandikwa kuhusu mada ........ 4

1.8 Misingi na Nadharia ........ 6

1.9 Mbinu za utafiti ........ 8

**SURA YA PILI ........ 10**

**MAWANDA YA UHAKIKI WA FANI ........ 10**

2.1 Utangulizi ........ 10

2.2 Dhana ya fani ........ 10

2.3 Msuko ........ 11

2.3.1 Msuko mkuu ........ 13

2.3.2 Msuko kinzani ........ 13

2.3.3 Msuko msago ........ 13

2.3.4 Msuko changamano ........ 13

2.3.5 Msuko rudufu ........................................................................................................ 14
2.4 Muundo ........................................................................................................ 14
2.4.1 Muundo wa ndani ........................................................................................................ 14
2.4.2 Muundo wa Ki-vitushi ........................................................................................................ 14
2.4.3 Muundo wa nje ........................................................................................................ 15
2.5 Mandhari ........................................................................................................ 17
2.6 Wahusika ........................................................................................................ 18
2.6.1 Jinsi ya kwanza ........................................................................................................ 18
2.6.2 Jinsi ya pili ........................................................................................................ 19
2.6.3 Jinsi ya tatu ........................................................................................................ 19
2.7 Matumizi ya lugha ........................................................................................................ 21
2.7.1 Uhuru wa kishairi ........................................................................................................ 23
2.8 Usimulizi ........................................................................................................ 31
2.9 Hitimisho ........................................................................................................ 32

**SURA YA TATU ........................................................................................................ 33**

**MSUKO, MUUNDO, MANDHARI NA WAHUSIKA ........................................................................................................ 33**

3.1 Utangulizi ........................................................................................................ 33
3.2 Msuko ........................................................................................................ 33
3.3 Muundo wa nje ........................................................................................................ 37
3.4 Mandhari ........................................................................................................ 39
3.5 Wahusika ........................................................................................................ 42
3.5.1 Mwana Hasina ........................................................................................................ 42
3.5.2 Rashidi ........................................................................................................ 44
3.5.3 Sultani ........................................................................................................ 46
3.5.4 Kijakazi ........................................................................................................ 47

3.5.5 Mchungaji/Saimu ........ 48
3.6 Hitimisho........ 48

**SURA YA NNE ........ 49**

**MATUMIZI YA LUGHA NA USIMULIZI........ 49**

4.1 Utangulizi........ 49
4.2 Uhuru wa kishairi........ 49
4.2.1 Ukiushi wa kimofolojia........ 49
4.2.2 Ukiushi wa kimsamiati........ 51
4.2.3 Ukiushi wa kisintaksia ........ 52
4.3 Tamathali za usemi ........ 52
4.3.1 Maswali ya balagha........ 52
4.3.2 Tashbihi........ 53
4.3.3 Takriri........ 54
4.3.4 Chuku ........ 55
4.3.5 Taswira........ 56
4.3.6 Uzungumzinafsia........ 58
4.3.7 Misemo........ 59
4.3.8 Kinaya ........ 60
4.3.9 Uhuishi ........ 60
4.3.10 Methali ........ 61
4.3.11 Nidaa ........ 61
4.3.12 Istiari........ 62
4.4 Usimulizi........ 62
4.5 Hitimisho........ 64

**SURA YA TANO ... 65**

**TATHIMINI NA MAPENDEKEZO ... 65**

5.1 Utangulizi ... 65

5.2 Muhtasari wa utafiti ... 65

5.3 Kuhusu malengo ya utafiti ... 66

5.4 Utathmini wa nadharia tete ... 67

5.5 Mapendekezo ... 68

**MAREJELEO ... 69**

# SURA YA KWANZA

## 1.1 Utangulizi

Fani ni ufundi wa kisanaa autumiao msanii katika kutoa ujumbe aliodhamiria kwa hadhira yake aliokusudia. Kwa hivyo, hiki kipengele ni muhimu sana katika fasihi. Huhusisha vipengele muhimu ambavyo huipa kazi ya sanaa muundo maalum. Vipengele hivi vyake vina utendakazi mkubwa katika kuwasilisha ujumbe uliodhamiriwa katika kazi ya kisanaa. Vipengele vya fani kama wanavyotaja Fokkema na Ibsch (1978) ni tamathali za usemi, ploti, maswali ya balagha na msamiati.

Katika utafiti wetu, tumejikita katika vipengele vitano vya fani. Vipengele hivi ni: Mtindo, muundo, wahusika na uhusika, msuko na mandhari. Tumerejelea *Utenzi wa Mwana Hasina na Rashidi Walii* uliotungwa na Saidi Abdullah Masud(1964) na kuhaririwa na Jan Knappert (1967).

Mtindo ni upekee wa uundaji wa kazi ya fasihi na hutofutiana baina ya msanii mmoja na mwingine kulingana na hisia za msanii huyo. Utofauti huu waweza kujitokeza kwenye uteuzi wa msamiati, tamathali za semi, mandhari, miongoni mwa mengine. Mtindo hurejelea mwandishi aliyehusika kwa maana upekee wake ndicho kile kinachoonekana kwenye kazi yake.

Muundo ni namna matukio katika kazi ya fasihi yalivyopangwa na kuleta mtiririko wa kazi ya fasihi. Kinachozingatiwa ni jinsi mtunzi alivyopanga kazi yake ili kuipa muwala na mshikamano faafu wa matukio. Hata hivyo, maoni ya Mbatiah (2001) kuhusu muundo ni kwamba, huu ni uhusiano wa elementi za kazi ya fasihi katika mpangilio dhabiti unaoshikamanisha elementi hizo, lakini sio lazima elementi hizi za kimuundo zionekane kijuujuu.

Mandhari huwa ni sura ya mahali, hususan jinsi panavyoonekana katika hali halisi ya maisha. Ni mahali ama wakati tukio la kifasihi lilipobuniwa na kutendeka. Mandhari huweza kuwa halisi au ya kufikirika. Mandhari husaidia katika kujenga dhamira, maudhui, usawiri wa wahusika na hutupa fununu ya falsafa ya mtunzi.

Wahusika na uhusika ni viumbe hai au visivyo hai vinavyobuniwa na msanii na kuwakilisha matendo, tabia na mienendo fulani ya watu katika kazi ya fasihi. Wahusika huweza kuwa watu, wanyama au mimea. Wahusika hawa huwa na sifa mbalimbali. Kwa mfano: Sifa za kimaandili, kiitikadi na kifalsafa.

Msuko ni mpangilio kamilifu wa matukio au visa katika kazi ya kifasihi. Msuko unaweza kuelezwa kama mtiririko wa vitendo na vitendo vinavyozuana. Kulingana na Njogu na Chimerah (1999) msuko ni mtiririko au mfululizo wa matukio yanayojenga hadithi na namna matukio haya yanavyosababishana.

*Utenzi wa Mwana Hasina na Rashid Walii* unahusu hadithi juu ya Sultan mmoja aliyekuwa na mtoto wa kike pekee. Alimtahadharisha asijiingize kwa matendo ya uzinifu ili asimwaibishe lakini hakufuata ushauri huo. Badala yake anashikwa na uchu wa mapenzi na kumwandama kijana ambaye ni mcha Mungu anayeitwa Rashidi ambaye hakuweza kunaswa na mtego wake. Jitihada zake zote za kumnasa zilipogonga mwamba, anaingilia uzinzi na vijana wachunga mbuzi na mwishowe akaishia katika lindi la maangamizi.

### 1.2 Tatizo la utafiti

Pamekuwa na mjadala kati ya wataalamu anuwai kuhusu dhana ya fani. Kwa upande mmoja, kunao wanaopendekeza kwamba katika uchambuzi wa kazi ya kifasihi, vipengele vya fani na maudhui visitenganishwe kwa sababu ni kama chanda na pete. Wataalamu hawa ni kama vile Mishra (2011) katika juzuu lake la fani na maudhui akimnukuu Kant anayesema kuwa, fani bila maudhui ni utupu nayo maudhui bila fani ni pofu na kudhihirisha kuwa huwezi kuchambua kimoja na kutenga kingine. Kwa hivyo, sharti vipengele vyote vishughulikiwe sawia.

Kwa upande mwingine, kuna wale wataalamu wanaoonelea kuwa kipengele cha fani kina mhimili wake na hivyo kinaweza kujisimamia kivyake. Wataalamu hawa ni kama vile wahakiki wa aina za tanzu wajulikanao kama Wanaaristoria au Watahakiki Wakichikago kama tunavyoona katika Mishra (2011). Wanadai kuwa kipengele cha fani hakiwezi kufungamanishwa na vipengele vingine kwa sababu kimejitosheleza.

Katika utafiti huu wetu, tumejikita kwa mwonoulimwengu wa wataalamu wa Kichikago wanaopendekeza kuwa kipengele hiki cha fani kinao uwezo wa kushughulikiwa kivyake. Tumerejelea *Utenzi wa Mwana Hasina na Rashid Walii* ambao tumepata ushahidi kuwa kipengele hiki hakijawahi kufanyiwa utafiti wa kina. Utenzi huu ulihaririwa tu na Jan Knappert (1967). Lengo letu ni kuchunguza kana kwamba madai haya yana mashiko. Tumetumia nadharia ya Urasimu wa Kirusi. Matokeo ya utafiti wetu yametarajiwa kuwafaidi wasomi, wachanganuzi wa maandishi ya kifasihi, wakufunzi na wapenzi wa kuandika kazi ya kisanaa inayojumlisha kipengele hiki kwa kina.

### 1.3 Madhumuni ya utafiti

i. Kubainisha vipengele mbalimbali vya fani ambavyo vimetumika katika *Utenzi wa Mwana Hasina na Rashid Walii.*
ii. Kutathmini mchango wa vipengele vya fani katika kuwasilisha maana katika *Utenzi wa Mwana Hasina na Rashid Walii.*

### 1.4 Nadharia tete

i. Vipengele vya fani katika *Utenzi wa Mwana Hasina na Rashid Walii*, ndivyo nguzo kuu iliyotumiwa katika ujenzi wa utenzi wenyewe.
ii. Vipengele vya fani vilivyotumiwa katika *Utenzi wa Mwana Hasina na Rashid Walii*, vimechangia pakubwa katika uwasilishaji wa maana katika utenzi huu.

### 1.5 Sababu za kuchagua mada hii

Tumechagua mada hii kwa sababu kadhaa. Kwanza, *Utenzi wa Mwana Hasina na Rashid Walii* ni miongoni mwa tenzi ambazo hazijawahi kufanyiwa utafiti wowote wa kiusomi. Utenzi huu ulitungwa na S.A. Masud katika mwaka wa (1964), na kuhaririwa na Jan Knappert (1967). Utenzi huu ni wa kale. Aidha, tuligundua kuwa kuna pengo kubwa la kiusomi linalohitaji kuzibwa.

Pili, *Utenzi wa Mwana Hasina na Rashid Walii* umetungwa kwa msamiati wa kale ambao hautumiki siku hizi. Aidha, utenzi umetumia mseto wa lahaja. Hali hii imefanya wasomaji wengi kuhofia kuusoma kwani huenda wasipate ujumbe uliodhamiriwa na mtunzi wa utenzi kwa sababu ya uchangamano wa lugha.

Kwa jumla, sababu zetu za kuchagua mada hii zimechangiwa na shinikizo za kiusomi. Ni matumaini yetu kuwa utafiti huu utasaidia pakubwa katika hazina ya uhakiki wa Tenzi za Kiswahili za Jadi, ambazo kulingana na Mutiso (1996:50) zinaogopwa na wanafunzi wengi hata wale ambao Kiswahili ni lugha yao ya kwanza. Tunawapa changamoto wasomi na wahakiki wa fasihi ya Kiswahili, kuhakiki vipengele vingine vya fasihi kama maudhui na dhamira katika utenzi huu.

**1.6 Upeo na mipaka**

Utafiti huu unahusu matumizi ya fani katika *Utenzi wa Mwana Hasina na Rashid Walii*. Ili kufanikisha utafiti wetu, tumetumia nadharia ya Urasimu wa Kirusi inayosisitiza uhakiki wa kifasihi ufanywe bila urejelezi wa nje. Kunga wanazozitumia wasanii katika uwasilishaji wa ujumbe ndio lengo letu. Kwa kuwa dhana ya fani ni pana na ina vipengele vingi, tumechagua kuhakiki vipengele vitano ambavyo ni msuko, muundo, mandhari, wahusika na mtindo ambapo tumeshughulikia matumizi ya lugha na usimulizi. Tumejadili namna vipengele hivi vya kifani vilivyotumiwa, uamili wake wa kiumbuji na mchango wake katika muundo wa kazi nzima. Pamoja na hayo, tumedurusu kazi mbalimbali za wasomi wengine ili kuelewa maoni yao kuhusu vipengele hivi vya fani na sisi tumechangia maoni yetu.

**1.7 Yaliyoandikwa kuhusu mada**

Mengi yameandikwa kuhusu dhana ya fani katika fasihi ya Kiswahili. Vilevile, kuna tahakiki kadhaa zilizofanywa kuhusu fani katika matini mbalimbali. Hata hivyo, hakuna mengi yalioandikwa kuhusu *Utenzi wa Mwana Hasina na Rashid Walii*. Utenzi huu ulihaririwa na Knappert.

Mwangangi (1996) alitafiti kuhusu, “Uhakiki wa Fani katika Tamthilia za Kitsao.” Alishughulikia *Uasi* (1980), *Malimwengu Ulimwengu* (1981), *Bibi Arusi* (1983), na *Tazama Mbele* (1981). Mchango wake ni kuwa vipengele ambavyo hujenga ujumla wa fani vinaonyesha upekee wa mwandishi na huonyesha bayana mtazamo wake. Anaendelea kusema kuwa fani hutawala uwasilishaji, ushikamano na uhusiano wa kuathiriana kwa viungo mbalimbali vya fasihi. Isitoshe, ametoa kauli kuwa, ujumla wa matumizi ya lugha, uumbuji wa wahusika, mpangilio wa vitushi, uchoraji wa mandhari ndio fani. Tumeunga mkono mawazo yake maanake

fani huchangia sana katika kufanikisha kazi ya kifasihi. Hata hivyo, sisi tumejikita katika ushairi wa *Mwana Hasina na Rashidi Walii* (1964).

Omwayo (1997) alishughulikia "Fani katika Ushairi wa Mwalimu Mbega." Alihakiki *Upisho wa Malenga* na *Dafina ya Malenga* akitumia pia nadharia ya Urasimu wa Kirusi. Alichukulia kuwa fani ina mchango mkubwa katika kufumbata malengo ya msanii. Tofauti na utafiti wetu ni kwamba, tumejikita katika uhakiki wa fani na ufaafu wake katika *Utenzi wa Mwana Hasina na Rashid Walii* katika kufanikisha uwasilishaji wa ujumbe wa mtunzi.

Njogu na Chimerah (1999) wanadai kuwa katika uhakiki wa ushairi ambao unajikita kwa fani, mhakiki afaa kuzingatia yafuatayo: Mpangilio wa maneno na semi katika shairi nzima. Katika utafiti wetu, tumeshughulikia yafuatayo: Mtindo, muundo, wahusika na uhusika, mandhari na msuko wa ushairi kwa jumla.

Kisilu (2003) ametafiti kuhusu, "Mwingiliano wa Fani na Maudhui katika ushairi wa Kithaka wa Mberia." Alijikita kwenye *Mchezo wa Karata* na *Bara Jingine*. Mchango wake katika utafiti wake ni kuwa uteuzi wa fani unachangia sana katika kubuni maudhui. Alitumia nadharia ya Umuundo. Utafiti wetu ni tofauti kwa sababu tumetumia nadharia ya Urasimu wa Kirusi.

Wesa (2005) ameshughulikia, "Uhakiki wa Fani katika *Utenzi wa Fatuma* na *Utenzi wa Siri li Asirali*." Mtafiti huyo alishughulikia vipengele mbalimbali vya fani ambavyo ametolea maelezo tu bila kuhakiki matumizi yake kwa kina. Katika utafiti wetu tumeshughulikia jinsi kunga hizi za fani zilivyotumiwa na ufaafu wake katika kazi hii. Aidha, tumetumia nadharia ya Urasimu wa Kirusi.

Lugwiri (2011) alishughulikia kipengele hiki cha fani huku akijikita kwa vipengele vifuatavyo: Istiari, Taashira na Tashbiha katika *Utenzi wa Tambuka*. Alitumia nadharia ya Mtindo. Katika kazi yake ameangazia dhana hizi tatu kwa kuonyesha aina zake na jinsi zilivyochangia katika kueleza dhamira ya mtunzi. Tofauti na utafiti wetu, tumetumia nadharia ya Urasimu wa Kirusi huku tukijikita kwa vipengele vifuatavyo: Muundo, mtindo, mandhari, wahusika na uhusika na msuko kwa kurejelea *Utenzi wa Mwana Hasina na Rashid Walii* na jinsi fani hizi zimefanikisha kuwasilisha ujumbe wa mtunzi.

Karanja (2014) aliandika kuhusu, “Matumizi ya Istiari na Tashbiha katika diwani *ya Sauti ya Dhiki.*” Katika kazi yake alishughulikia matumizi ya lugha. Zaidi ya hayo, ametumia nadharia ya Mtindo. Kama nilivyotaja hapo awali, tumetumia nadharia ya Urasimu wa Kirusi katika utafiti wetu. Pia tumeshughulikia vipengele vitano vya fani ambavyo ni: Mtindo, muundo, wahusika na uhusika, mandhari an msuko.

**1.8 Misingi na Nadharia**

Katika utafiti wetu tumetumia nadharia ya Urasimu wa Kirusi. Wamitila (2002) anaeleza kuwa nadharia ya Urasimu wa Kirusi inahusishwa na wanafunzi wa fasihi kama: Boris Elchenbaum, Roman Jakobson, Victor Shklovsky na wengine. Nadharia hii iliibuka kupitia tapo lililokuja kujitambulisha awali baada ya mzozo wa Kihistoria na mapinduzi ya utawala wa Urusi (1917) takriban zaidi ya mwongo mmoja uliofuata.

Mbatiah (2001) anasema kuwa nadharia hii ya uhakiki iliibuka mjini Moscow katika miongo miwili ya kwanza ya karne ya ishirini. Kwa hivyo, chanzo cha nadharia hii ni Urusi. Nadharia hii pia huitwa Urasimu wa Kirusi. Nadharia hii hujihusisha na matumizi ya fani katika uwasilishaji wa kazi ya mtunzi.

Watetezi wa nadharia hii walihamia Prague katika nchi ya Czechoslovakia. Mwelekeo wa nadharia hii ni kuwa, fasihi ni matumizi ya kipekee ya lugha na ndiyo huzua kile ambacho waasisi wananadharia hii walikieleza kama Oistranenia. Walichomaanisha ni kuwa, jinsi fasihi inavyotumia lugha husawiri upya mitazamo ya maisha kwa njia ambayo inaondoa mikabala inayozoeleka na msomaji wa kazi husika.

Nadharia ya Urasimu wa Kirusi ilianzishwa wakati ambapo kulikuwa na harakati za kimapinduzi katika nchi ya Urusi, yaliongozwa na Lenin, V.I. yaliyodhamiriwa kuanzisha utawala wa kijamaa. Wakati huo makundi mawili yaliibuka. Kundi moja liliunga mkono mapinduzi likisema kwamba fasihi haiwezi kutenganishwa na jamii. Aidha, walidai kuwa hatuwezi kuitalii fasihi bila kuihusisha na jamii.

Wanaurasimu walipinga hoja hii wakisema kwamba fasihi ni tenge na jamii na inajitegemea. Miongoni mwa waasisi wa nadharia hii ni Roman Jakobson, Boris Tomashevsky, Boris Eichenbaum, na Victor Shklousky. Wananadharia hawa walijigawa katika makundi mawili.

Kundi la kwanza lilijulikana kama kundi la Isimu la Moscow. Kundi hili liliongozwa na Roman Jakobson katika mwaka wa 1915 (Fokkema na Ibsch, 1978). Wengine katika kundi hili walikuwa ni Brik, Boris na Tomashevsky (Buchbinder, 1991).
Kundi la pili lilijulikana kama Chama cha Mtalaa wa Lugha ya Kishairi. Miongoni mwa wanachama wa kundi hili ni Boris Eikhenbaum wakiongozwa na Victor Shklovsky katika mwaka wa 1916 (Buchbinder, 1991:77). Kundi hili lilisisitiza ya kwamba kazi ya kifasihi ni toshelevu na haikuhitaji urejelevu wa nje ili kuibua maana yake. Shklovsky anasema kuwa umbo kamili la kazi ya kifasihi hujitegemea katika kuibua maana bila kurejelea mambo yaliyo nje ya matini husika. Eikhenbaum kama anavyonukuliwa na Buchfinder (1991:81), anasema kwamba, "Vijenzi mbalimbali vya kazi ya kifasihi hutegemeana ili kuibua maana." Wananadharia hawa walikubaliana kuwa fani katika kazi ya kifasihi huibua maana fulani na pia aina mbalimbali za fani huwa na maana tofauti tofauti. Katika utafiti wetu tumerejelea maudhui pale ilipotulazimu ili kufafanua fani. Fokkema na Ibsch (1978) wanataja viungo vya fani kuwa: Tamathali za usemi, ploti, maswali ya balagha na msamiati. Lengo kuu la Wanaurasimu lilikuwa ni kuchunguza kazi za fasihi Kisayansi na kuhimiza umuhimu wa fani.

Mambo muhimu yaliyopewa uzito katika nadharia hii ni:
Wamitila (2003) anasema kulikuwa na msisitizo mkubwa kuhusu swala la fani katika fasihi. Hawakutilia mkazo maudhui ya kazi fulani ya kifasihi. Wazo hili limekuwa muhimu sana katika utafiti wetu. Tumetilia mkazo zaidi jinsi viungo mbalimbali vya fani vimeungana kuibua maana fulani. Tumechunguza jinsi viungo kama vile: Msamiati, tamathali za semi, msuko, mtindo, wahusika na mandhari vinavyochangia kuibua maana katika *Utenzi wa Mwana Hasina na Rashid Walii*.

Pili, Wanaurasimu wa Kirusi walichukulia fani kuwa kiungo kikamilifu katika kufafanua kazi za fasihi. Wazo hili pia limekuwa muhimu sana kwetu kwa sababu tumeshughulikia fani kama kiungo kikamilifu. Tumechukulia utendi huu kama mfumo wenye viambajengo mbalimbali na kila kiambajengo ni muhimu katika kuwasilisha ujumbe katika kazi nzima.

Tatu, wahakiki hawa walitilia mkazo mkubwa kwenye suala la kutalii fasihi Kisayansi. Katika utafiti wetu tumechunguza sifa za kifasihi ambazo ni za kijumla. Sifa hizi ni kama vile uwezo wa mtunzi kubuni mbinu mpya za kubuni kazi yake. Maana mtunzi wa kazi ya kifasihi hutumia

mbinu mbalimbali katika kufanikisha kazi yake na anapofaulu katika kufanya hivyo, analeta athari kwa msomaji.

Nne, wanaurasimu waliamini kwamba mwandishi wa kazi fulani ya Kifasihi hana nafasi kubwa katika uhakiki wa kazi ya fasihi. Wanampa mhakiki wa kifani uhuru wa kuhakiki bila kujishughulisha na mawazo ya mwandishi. Katika utafiti wetu, tumetathmini maana inayoibuliwa na fani fulani pale inapotumika na kuchunguza kama inafaa au haifai. Wazo hili limetupa uhuru wa kutoa mchango wetu kama wahakiki kuhusu jinsi fani mbalimbali zilivyotumika katika *Utenzi wa Mwana Hasina na Rashid Walii.* Omwayo (1997) anasema kuwa nadharia ya Urasimu inalenga kutathmini fasihi kwa kuchunguza fani yake; namna inavyofanya kazi. Sababu hizi zote ndizo zilizotufanya kuamini kuwa nadharia hii ndio inafaa katika utafiti wetu.

**1.9 Mbinu za utafiti**

Katika mbinu za utafiti, tumefafanua mahala pa utafiti, uteuzi wa sampuli, ukusanyaji data, uchanganuzi wa data na uwasilishaji wa data. Katika kila mojawapo wa vipengele hivi, tumefafanua mambo kadha ambayo tumejishughulisha nayo.

Utafiti wetu umekuwa wa kimaktaba kwa kiasi kikubwa ili kupata maandishi yanayohusiana na mada yetu tuliyoishughulikia. Tumerejelea viada na makala ambayo yametutolea maelezo kuhusu utanzu tunaoutafiti wa fasihi andishi hasa ushairi. Viada na makala haya yametupa ufafanuzi kuhusu mihimili ya nadharia ya Urasimu wa Kirusi ambayo tumetumia katika utafiti wetu. Aidha, tumerejelea tasnifu mbalimbali zinazohusiana na mada yetu ya fani. Fauka ya hayo, tumesoma makala ambayo yaliandikwa na wasomi wengine kuhusu fani. Makala haya yametupatia mwongozo katika ufafanuzi wa utafiti ambao tulishughulikia.

Sampuli ambayo tumeteua ni sampuli lengwa ambayo ni *Utenzi wa Mwana Hasina na Rashidi Walii*. Kwa mujibu wa Mugenda na Mugenda (1999:56) aina hii ya sampuli hutumika katika utafiti unaokusudiwa kupata habari za kina na bila kujumlisha. Kwa kurejelea maelezo haya, tumechagua *Utenzi wa Mwana Hasina na Rashidi Walii* na tumeshughulikia kipengele cha fani kwa kujikita kwa vipengele vifuatavyo: Msuko, muundo, mandhari, wahusika na uhusika na matumizi ya lugha.

Data tuliyoipata tumeichanganua kulingana na malengo ya utafiti pamoja na mihimili ya nadharia ya Urasimu wa Kirusi. Kwa kutumia msingi wa nadharia hii, tumechanganua vipengele vifuatavyo vya fani: Msuko, muundo, mandhari, wahusika na uhusika na mtindo huku tukijikita kwa matumizi ya lugha na usimulizi katika *Utenzi wa Mwana Hasina na Rashidi Walii*.

Baada ya kukusanya data na kuichanganua, uwasilishaji wa matokeo tumeufanya kwa njia ya maelezo hasa kuhusu vipengele vifuatavyo vya fani: Msuko, muundo, wahusika na uhusika, mandhari na mtindo huku tukijikita katika matumizi ya lugha na usimulizi katika *Utenzi wa Mwana Hasina na Rashidi Walii*.

# SURA YA PILI

# MAWANDA YA UHAKIKI WA FANI

## 2.1 Utangulizi

Katika sura ya kwanza tumeshughulikia mambo yanayohusiana na utangulizi wa utafiti wetu. Katika sura hii, tumejadili mawada ya kinadharia ya fani. Zaidi ya hayo, tumejadili dhana ya fani na kuvibainisha viambajengo vyake mbalimbali na kuonyesha uainishaji wake. Tumetoa mifano kutoka katika ushairi wa Kiswahili. Dhana ya fani ni pevu na inajumulisha vipengele vingi sana. Tumejadili tu vipengele ambavyo tumevitumia katika *Utendi wa Mwana Hasina na Rashidi Walii* katika sura zijazo.

## 2.2 Dhana ya fani

Dhana ya 'fani' katika fasihi imeelezwa na kufafanuliwa na wataalamu mbalimbali. Miongoni mwa waandishi hawa ni Njogu na Chimerah (1999), Mbatiah (2001) na Wamitila (2002, 2003). Watalamu hawa wana maoni anuwai kuhusiana na kipengele hiki. Maoni haya ni kama yafuatayo:

Njogu na Chimera (1999) wanaeleza fani kama ufundi wa kisanaa autumiao mwandishi katika kuwasilisha kazi yake kwa hadhira. Wamitila (2003) anaeleza kuwa fani hutumiwa kueleza muundo au mpangilio wa kazi fulani ya kifasihi au hata sehemu zake. Fani hueleza mbinu na mtindo wa kuyawasilisha yaliyomo au maudhui. Mbatiah (2001) anasema kwamba dhana ya fani ina maana mbili. Kwanza, ni jumla ya vipengele vya kimtindo na kisanaa katika kazi ya kifasihi vinavyojenga kiunzi cha kuubebea ujumbe au maana mahususi. Pili, ni kategoria ya fasihi, yaani utunzi kama ushairi, drama na riwaya.

Kwa kurejelea wanavyosema kuhusiana na uchunguzi wetu, wataalamu hawa watatu wanaelekea kukubaliana na maana ya kwanza ya Mbatiah (2001) kuwa, fani ni vipengele vya kimtindo na kisanaa vinavyojenga kiunzi cha kuubebea ujumbe na maana mahsusi. Kimsingi, kazi za fasihi huwa zimegawika katika sehemu mbili kuu: Maudhui na fani. Maudhui ni masuala mbalimbali yanayozungumziwa na mtunzi katika kazi ya fasihi. Maudhui aidha huelezwa kama yaliyomo. Kwa upande mwingine, fani huwa ni vipengele vya kisanii vitumiwavyo kuwasilisha maudhui.

Kando na kuyawasilisha maudhui, fani huwa na uamilifu wa kuupa utungo wa kifasihi umbo mahususi. Umbo lenyewe laweza kuwa la ndani au nje. Katika tungo za kishairi, umbo la ndani hujengwa kwa vipengele vya fani kama vile: Matumizi ya lugha, wahusika, mandhari, msuko, usimulizi na toni miongoni mwa vingine. Umbo la nje hujengwa kwa vipengele vya fani kama vile: Beti, mishororo, mizani na vina.

Utafiti wetu umehusu uchanganuzi wa mambo haya yote. Wataalamu wa nadharia ya Urasimu wa Kirusi wanasisitiza na kutilia mkazo uhakiki wa kifani katika kufasiri matini na kupimia kufaulu au kufeli kwa mtunzi katika kazi yake ya usanii. Kwa vile vipengele vya fani ni vingi, tumeshughulikia baadhi yavyo vikiwemo: Msuko, wahusika na uhusika, muundo, mandhari na mtindo, ambapo katika mtindo tumejikita katika matumizi ya lugha na usimulizi pekee.

**2.3 Msuko**

Msuko ni kipengele muhimu sana cha fani katika kazi ya fasihi. Njogu na Chimerah (1999) wanasema kuwa msuko ni mtiririko au mfululizo wa matukio yanayojenga hadithi na namna matukio hayo yanavyosababishana. Wataalamu hawa wanaendelea kueleza kuwa msuko unaweza kuelezwa kama mtiririko wa vitendo na namna vitendo hivyo vinavyozuana.

Wamitila (2003) anasema kuwa msuko ni dhana ya kifasihi ambayo hutumiwa kurejelea mpangilio wa matukio yanayopatikana katika hadithi, na huhusisha matendo ya nguli na jinsi yanavyowathiri wahusika wengine. Msuko hueleza namna matukio haya yanavyofuatana kiusababishi. Wamitila anaendelea kueleza kuwa istilahi hii ilitumiwa kwa mara ya kwanza na Aristotle alipoongea kuhusu muundo wa tanzia. Baadhi ya sifa za kimsingi zinazohusiana na msuko unaojenga kazi ya fasihi ni pamoja na ukubalifu, taharuki, mgogoro, matumaini au matarajio, usababishi na tokeo, mantiki, mshutukizo na mvuto.

Kwa upande mwingine, Ngara (1985) anasema kuwa uti wa mgongo wa kazi ya kifasihi ni msuko. Maoni haya yana maana kuwa msuko huweka pamoja vipengele vingine vya kazi ya kifasihi na kuvipa muundo. Kufuatia fafanuzi za wataalamu hawa, tunapata mambo muhimu yanayoeleza msuko:

Kwanza, kuna kuzingatia mpangilio. Ni lazima msanii ateue na kuyapanga matukio yake kiwakati na pia kuwe na uhusiano wa kiusababishi na kutegemeana katika suluhu. Lazima matukio yapangwe kulingana na azma ya msuko wa kazi ya msanii.

Pili, kuwe na mfululizo wa vitendo. Vitendo vyapaswa vianzie mwanzoni mwa kazi inayohusika na kuendelea kwa uhusiano wa kimantiki hadi kufikia mwisho wa kazi yenyewe. Tukio moja haliwezi kuunda msuko mzima. Kwa hivyo, lazima kuwepo mwanzo wa matukio, kati na mwisho katika mwingiliano wa nguvu zinazokinzana na mara nyingi hii humaanisha kuwepo visa vitatu au zaidi. Matukio hukua moja baada ya jingine. Tukio la pili likifuata kwa uhusiano wa kiusababishi kutoka kwa tukio la kwanza na la tatu likifuata kwa uhusiano huo kutoka kwa la pili. Hadithi yenye msuko wa matukio uliofungamana, tukio moja likiondolewa tu, basi hadithi nzima itakuwa imeumbuliwa. Ni muhimu kutambua kuwa, pia matukio ya mwanzo yanaweza kupelekwa mwisho na ya mwisho kuletwa mwanzo. Isitoshe, msuko mkuu waweza kuwa na mingine midogo midogo. Msuko wa aina hii huwa changamano.

Tatu, kuwe na uhusiano wa vitendo ambao huwa ni tokeo la mwingiliano wa nguvu na nguvu nyingine. Yamkini pasipo mgogoro au ukizani, msuko au ploti hautakuwepo. Nazo nguvu za ndani na za nje lazima ziweze kuonyesha ukinzani. Ukinzani ndio unaofungamanisha tukio moja kwa tukio lingine. Pamoja na hayo, ndio unaimarisha uhusiano wa kiusababishi unaojenga mapambano. Mapambano ya nguvu kwa nguvu. Wakati mwingine hufika kilele katika tukio moja na baada ya hapo, kunaweza kuwa na taharuki.

Murage (2011) anasema msuko ukiwa mpangilio wa matukio hulenga kwenye maisha huku ukichagua wahusika wachache, migogoro michache na visa vichache kutoka kwa kapu kubwa lenye sampuli nyingi. Uchaguzi huu huwa ni wa vitu vyenye mshikamano wa pamoja na unalenga mwisho mmoja. Msuko hujitokeza vizuri katika ushairi hasa utendi kwa sababu ya kipengele cha hadithi.

Wamitila (2003), ameainisha misuko mbalimbali: Msuko mkuu, msuko kinzani, msuko msago, msuko changamano au wa kioo na msuko rudufu. Kwa sasa tumefafanua aina hizi za misuko huku tukitoa mifano kutoka kwa tenzi zingine. Hata hivyo, tumerejelea *Utenzi wa Mwana Hasina na Rashid Walii* katika sura zijazo.

### 2.3.1 Msuko mkuu

Msuko mkuu unahusu hadithi kuu katika kazi ya fasihi. Msuko mkuu hupatikana pale ambapo kazi ya fasihi ina msururu wa hadithi ambazo kila moja ya hadithi hizo inatambulika. Kimsingi, msuko mkuu huhusisha matendo na maelezo kuhusu mhusika mkuu katika kazi ya fasihi. Kwa mfano, katika *Utenzi wa Mwana Fatuma*, msuko mkuu ni ule wa harusi ya Fatuma na Ali. Mtunzi anasimulia vijihadithi vingine kama vile: Sifa za Mtume Muhammadi na sifa nzuri za Fatuma. Mtunzi anazunguka hapa na pale badala ya kutueleza bayana kuhusu harusi ya Fatuma na Ali moja kwa moja. Aidha, anaeleza mauti ya Khadija, pia anasimulia kuhusu sifa za Mtume Muhammadi.

### 2.3.2 Msuko kinzani

Kwa mujibu wa Wamitilia (2003) msuko kinzani hutumiwa kurejelea matukio yanayotendwa na kumzunguka mhusika mkuu katika kazi ya fasihi. Msuko huu hueleza matukio ambayo yanakusudia kufikia lengo tofauti na lile la msuko mkuu. Msuko wa aina hii huhusishwa na mhusika anayepigana na mhusika mkuu. Mhusika wa aina hii hutenda matendo yanayoonyesha kupinga au kuasi mwelekeo unaochukuliwa na mhusika mkuu. Kwa mfano, katika *Utenzi wa Ayub*, msuko kinzani unahusu matukio na matendo yanayomzunguka Ibilisi ambaye ni mpinzani wa Ayubu.

### 2.3.3 Msuko msago

Kulingana na Wamitila (2003) msuko msago pia huitwa msuko sahili. Msuko msago ni aina ya msuko ambao ni wa moja kwa moja bila ya kuwa na matumizi ya mbinu rejeshi. Hutiririka kuanzia mwanzo hadi mwisho. Mara nyingi, msuko wa aina hii hupatikana katika tungo fupi kama vile hadithi fupi na vilevile mashairi. Msuko wa aina hii unapatikana katika *Utenzi wa Ayub*. Katika utenzi huu, hali ya Ayub ya kumcha Mungu inasababisha Ibilisi kumuomba Mungu ruhusa amjaribu kwa mali na afya yake. Kuugua kwa Ayub kwa muda mrefu kunapelekea Rehema kutafuta kazi kwa majirani ili apate chakula kisha Ibilisi anamletea Ayubu majaribu mengi.

### 2.3.4 Msuko changamano

Kulingana na Ngara (1985) msuko huu hujulikana kama msuko wa kioo. Msuko huu una urejelezi mwingi sana. Msuko wa aina hii huwa na kipengele cha wakati na vipengele kama vile:

Wahusika na usimulizi. Aidha, lazima kuwepo na mahusiano ya vipengele hivi na matukio ambayo yanatendwa katika nyakati tofautitofauti. Nyakati hizi zinapowasilishwa katika hadithi, lazima ziwe katika wakati uliopo, uliopita na hata ujao. Muundo huu ndio huleta urejeshi katika hadithi. Katika mashairi hupatikana katika tenzi ndefu kama vile *Utenzi wa Masahibu*.

### 2.3.5 Msuko rudufu

Murage (2011) anasema msuko rudufu ni msuko ambao unahusisha zaidi ya msuko mmoja katika kazi ya kifasihi. Misuko inayopatikana katika kazi ya aina hii inafaa kuwa na nafasi sawa. Yaani hadithi mbalimbali zinazopatikana na kila moja ikatambuliwa waziwazi. Mfano wa msuko rudufu unapatikana katika *Utenzi wa Khatilifu* ambapo kuna aina mbili za misuko. Aidha, kuna msuko changamana na msuko kinzani.

## 2.4 Muundo

Wamitila (2003) anasema kuwa muundo unaweza kuwa wa ki-vitushi, muundo wa ndani ama muundo wa nje. Maoni yetu ni kwamba muundo ni mpangilio na mtiririko wa matukio katika kazi za kifasihi.

Mbatiah (2001) anaeleza kuwa, muundo ni uhusiano wa elementi za kazi ya fasihi katika mpangilio dhabiti unaozishikamanisha elementi hizo. Hata hivyo, si lazima elementi za kimuundo ziweze kuonekana kijuujuu. Baadhi ya elementi hizi huwa za kindani. Kwa hivyo, lazima hadhira isome kazi inayohusika ili kubaini na kuelewa elementi hizo. Hali hii husababisha kuwepo kwa aina mbili kuu za miundo katika kazi za kifasihi, muundo wa ndani na muundo wa nje.

### 2.4.1 Muundo wa ndani

Muundo wa ndani ni aina ya muundo wa kazi ya kifasihi ambao hauwezi kuonekana kwa macho. Dhana hii hutumika kueleza sifa za ndani za kazi ya fasihi. Kwa mfano, jinsi sehemu mbalimbali zinavyohusiana kama vile: Wahusika na mandhari, mtazamo na mandhari na wahusika na matumizi ya lugha. Kwa mfano, katika *Utenzi wa Ayub,* Ibilisi anahusiana na Mungu kumjaribu Ayub.

### 2.4.2 Muundo wa Ki-vitushi

Muundo wa ki-vitushi ni dhana inayotumiwa kueleza kazi ya kinathari, ambayo inahusisha hadithi au vijihadithi vinavyoelekea kujitegemea, lakini vina kiunganishi fulani

kinachoviunganisha. Kimsingi, muundo katika mtazamo huu unaingiliana na dhana ya msuko. Kigezo kinachotumiwa ni cha hadithi au visa.

### 2.4.3 Muundo wa nje

Muundo wa nje ndio hurejelewa kama umbo la kifasihi. Hii ni aina ya muundo wa kazi ya kifasihi ambao huonekana na kutambulika kwa kutazama tu. Aidha, muundo huu unahusiana na urefu, mgawo, sura au maonyesho ya kimpangilio. Hadhira inaweza kutambua vijenzi vya muundo wa nje wa shairi kwa kulitazama tu. Si lazima walisome shairi hilo. Hoja hii inaelezwa vizuri na Mohammed (1995) anaposema kuwa, umbo linajengwa na vipengele vinavyoungana pamoja kujenga kitu kimoja kikuu. Mohammed anaendelea kueleza kuwa katika shairi vipengele hivi ni: Beti, vipande, mishororo, mizani, vina na kibwagizo.

#### 2.4.3.1 Beti

Murage (2011) beti ni kifungu cha mshororo katika ushairi. Pia, ni migao mbalimbali. Migao hii yaweza kulinganishwa na aya za tungo za kinathari. Beti za mashairi ya kiarudhi huwa na migao ya idadi maalum ya mishororo. Shairi linaweza kuwa na idadi yoyote ya beti ilmuradi tu litekeleze azma yake. Baadhi ya mashairi huwa yana beti nyingi ilhali mengine huwa na beti chache. Tenzi aghalabu huwa na beti nyingi. Kwa mfano,*Utenzi wa Masahibu* una beti elfu moja na arobaini na sita.

#### 2.4.3.2 Mishororo

Mishororo ni mistari ambayo hupatikana katika kila ubeti wa shairi. Idadi ya mishororo ni mojawapo ya vipimo vya kuainisha mashairi katika aina mbalimbali. Kulingana na kaida za mashairi ya jadi, kila shairi sharti liwe na idadi maalum ya mishororo. Kwa mfano, shairi lenye mishororo minne katika kila ubeti huitwa tarbia. Tenzi nyingi huwa na mishororo minne katika kila ubeti. Hivyo, tenzi ni aina ya mashairi ya tarbia. Ufuatao ni mfano wa ubeti wa kwanza wa *Utenzi wa Masahibu*:

Pili lake sultani
Ni mchache wa imani
Kuwatesa maskini
Kwake haoni vibaya.

Ubeti huu una mishororo minne inayothibitisha kuwa utenzi huu ni aina ya tarbia.

#### 2.4.3.3 Vipande

Tambasi (2011) anasema vipande ni migawo inayopatikana katika mishororo ya tungo za kishairi. Kunayo mashairi yenye mgao mmoja, miwili na hata mitatu. Mashairi huru hayana vipande vya mishororo vyenye ubainifu kama mashairi ya jadi. Kwa upande mwingine, mashairi ya kimapokeo yana sifa ya kugawika kwa mishororo kama mojawapo ya kaida zake. Kwa mfano, aina ya mashairi ya ukawafi huwa na vipande vitatu katika kila mshororo ilhali beti za tenzi huwa na kipande kimoja pekee.

#### 2.4.3.4 Mizani

Murage (2011) anaeleza mizani ni idadi ya silabi katika mshororo wa shairi. Mizani inaweza kuwa na silabi za irabu moja tu au iwe ni silabi yenye muungano wa konsonanti moja au zaidi na irabu moja. Idadi ya mizani katika kila mshororo huweza kutofautiana kutoka aina moja ya shairi hadi nyingine. Kufuatia kigezo hiki cha idadi ya mizani katika mshororo wa kila ubeti, tunapata aina tofauti za mashairi kama vile: Kisarambe (mizani kumi na moja), tendi (mizani 6,8,11), gungu (mizani 10) na mengineyo. Haya ni kulingana na Wamitila (2008) na Abed (1954:25).

#### 2.4.3.5 Vina

Murage (2011) anasema vina ni aina ya urudiaji wa sauti unaotokea mwishoni mwa mishororo katika tenzi. Kulingana na Wamitila (2008) urudiaji wa silabi unaotokea katika sehemu ya mwanzo wa mishororo unaweza kujumulishwa hapa kwa kuwa kimsingi, unaonyesha mfanano wa mizani. Hata hivyo, wazo hili la Wamitila tungependekeza lifanyiwe utafiti zaidi. Ufuatao ni mfano wa vina katika *Utenzi wa Masahibu*:

Huwaandama ndai<u>ni</u>
Huwatesa mask<u>ini</u>
na warudipo nyumba<u>ni</u>
huzidi kuwaonea

#### 2.4.3.6 Kibwagizo

Istilahi hii hurejelea mshororo wa mwisho wa kila ubeti wa shairi fulani ambao umerudiwa kutoka ubeti mmoja hadi mwingine. Kibwagizo hubeba ujumbe maalum wa shairi hilo na husisitiza ujumbe huo. Kwa hivyo, kibwagizo huwa ni muhimu sana katika kufasiri dhamira ya shairi husika. Hata hivyo, si mashairi yote yaliyo na kibwagizo. Mashairi yasiyo na kibwagizo huwa na kiishio.

## 2.5 Mandhari

Gill (1985) anafafanua mandhari kama neno pana linalohusisha mahali ambapo wahusika wamewasilishwa na muktadha wa kijamii. Wahusika ni kama vile: Familia, marafiki, matabaka, tamaduni na imani na kaida za jamii kitabia. Mandhari huchangia katika kueleza mengi kuhusu sifa na tabia za wahusika, hali waliyomo na kutambua maudhui yaliyo katika kazi ya fasihi.

Wamitila (2003) anasema kuwa mandhari ni dhana ambayo hurejelea wakati na mahali pa hadithi au tamthilia. Ni mazingira ya utendaji wake au usimulizi wake. Aidha, dhana hii hutumiwa kueleza mazingira ya kijamii na kielimu wanakojikuta wahusika wa fasihi.

Mandhari katika ushairi huibuka na kwenda pamoja na matukio pasi na maelezo ya kina ya mandhari. Mandhari yafaa yahusishwe pamoja na mila na itikadi za jamii, dini na utamaduni na sio kuhusishwa na mazingira tu katika tenzi. Mara nyingi, wasomaji wa ushairi hupenda kuona mandhari yanayoweza kutambulika lakini hili haliwezekani katika kazi ambazo haziandikwi katika misingi ya uhalisia.

Mandhari huweza kuhusisha mahali kama vile: Msituni, porini, ahera, duniani, pangoni, miongoni mwa mengine. Pamoja na haya, mazingira nayo humwezesha msomaji kuelewa taswira ya msanii. Mazingira yaweza kuwa ya kivita, kisiasa, kidini, kimapenzi, kijamii, kimapinduzi na kiuchumi miongoni mwa mengine. Wakati mwingine mandhari huweza kuwa ya ukinzani au usambamba na msanii hutumia haya kuwasilisha ujumbe wake. Aidha, anaweza kuwasilisha maisha ya umaskini na ya utajiri.

Gill (1985) na Wamitila (2002) wamezungumzia kuhusu upana wa mandhari. Wamesema kuwa mandhari si mazingira tu bali hurejelea masuala mengi yakiwemo itikadi, mila, desturi, jamii na vilevile elimu. Kwa hivyo, mandhari huweza kuhamishwa katika mazingira tofauti kulingana na muktadha. Kwa mfano, tukiangazia tenzi kama vile *Siri li Asirali* wenye mandhari ya kivita na Miraji wenye mandhari ya mbinguni ni bayana kuwa mandhari huwa mapana.

Vitengo vinavyotengeneza mandhari ni kama vile: Hali ya Kijiografia hali ya Kihistoria na au kipindi maalum hasa msimu wa mwaka. Mandhari pia hujengwa kwa mazingira ya kijumla ya mhusika, yaani hali yao ya kidini, kiakili na kijamii. Kwa kuangazia maoni ya wataalamu tuliowataja hapo juu kuhusu dhana ya mandhari, tumepata kuwa mandhari ni mahali na wakati

ambapo matukio ya kifasihi hufanyika. Mandhari huweza kuwa halisi au ya kufikirika. Mandhari pia husaidia katika kujenga dhamira, maudhui, usawiri wa wahusika na hutupa fununu ya falsafa ya mtunzi.

### 2.6 Wahusika

Wahusika ni viumbe wanaopatikana katika kazi yoyote ile ya kifasihi. Viumbe hawa huwa ni sehemu ya kazi nzima. Pili, wahusika ni binadamu wanaopatikana katika kazi ya kifasihi na ambao wana sifa za kimaandili, kitabia, kiitikadi na kifalsafa ambazo hutambuliwa na wanayoyasema na wanayoyatenda. Wahusika huweza kutambulishwa pia na maelezo ya mhusika au msimulizi. Kuna jinsi mbalimbali za kuainisha aina za wahusika. Kwa mujibu wa Njogu na Chimerah (1999) kuna jinsi tatu zakuanisha wahusika. Jinsi hizi ni kama zifuatazo:

#### 2.6.1 Jinsi ya kwanza

##### 2.6.1.1 Mhusika mkwezwa

Huyu ana sifa za kiutendaji. Aidha, ni hodari na shujaa na kama wahusika wa fasihi simulizi ni stadi na anatumia mantiki kufikia kauli na uamuzi. Pia, ameinuliwa lakini habadiliki licha ya mpito wa wakati.

##### 2.6.1.2 Mhusika wa kimapinduzi

Huyu anaelewa historia, siasa, mazingira na hali ya jamii yake. Yuko radhi kujitoa mhanga kubadilisha maisha ya wanyonge. Ana itikadi kali na msimamo thabiti.

##### 2.6.1.3 Mhusika wa kisaikolojia

Huyu anakumbana na matatizo mengi ya kijamii na anaibuisha hisia za huruma kwa wasomaji. Mfano mzuri ni Ayub katika *Utenzi wa Ayub*. Aidha, anakubana na shida nyingi kama vile, kupoteza mali yake yote. Shida hizi ambazo anapata zinaibua huruma kutoka kwa msomaji.

##### 2.6.1.4 Mhusika jumui

Ni mhusika wengi – katika – mmoja. Hupatikana zaidi katika fasihi ya kidhanaishi. Mhusika huyo mmoja anakuwa na sifa za wahusika wengi. Anatumiwa kuonyesha fujo za maisha.

### 2.6.2 Jinsi ya pili

Aidha, Njogu na Chemerah (1999) hawa wanazidi kusema kuwa katika uhakiki wa mashairi, tunaweza pia kuwagawanya wahusika katika matapo matatu ambayo kupitia kwayo, dhamira na maudhui ya mwandishi hujibainisha. Matapo haya ni: Wahusika wakuu, wahusika wasaidizi na wahusika wajenzi

#### 2.6.2.1 Wahusika wakuu

Wahusika wakuu ndio nguzo kuu ambayo husheheni hadithi nzima. Wahusika hawa huisukuma hadithi mbele kwa sababu matendo na migogoro yote muhimu inawahusu. Dhamira kuu ya mwandishi hujitokeza kupitia kwao na msimamo wa mwandishi kuhusu dhamira, matukio na vitushi vya hadithi hujibainisha kupitia kwa matendo na maneno yao. Mwandishi humkuza atakavyo huku akimfanya atangamane na wahusika wengine ili kufaulisha kazi yake. Kwa hivyo, wahusika wakuu hawawezi kufaulu pasi na kuhusiana na wengine ili kuonyesha hali ilivyo. Hata hivyo, wao ndio hutawala sehemu kubwa.

#### 2.6.2.2 Wahusika wasaidizi

Wahusika wasaidizi wanatumiwa ili kumsaidia msomaji amwelewe vyema mhusika mkuu. Yaani, kupitia maingiliano baina ya mhusika mkuu na mhusika msaidizi, tunapata mwanga zaidi kuhusu hulka ya mhusika mkuu. Huwasaidia wahusika wakuu kujenga kazi na kusaidia katika kuupitisha ujumbe wa mwandishi.

#### 2.6.2.3 Wahusika wajenzi

Hawa wamewekwa kwa lengo la kukamilisha dhamira na maudhui ya mwandishi. Hali kadhalika, wanajenga wahusika wasaidizi na wakuu. Kundi hili ndilo hasa linalowakilisha jamii pana na matendo yao aghalabu huonekana kama kwamba ni ya pembezoni. Wao hawatokei sana kama wahusika wasaidizi au wakuu. Husaidia kudokeza au kuongeza nguvu kwa masuala yanayoendelezwa na mhusika mkuu kwa usaidizi wa wahusika wasaidizi.

### 2.6.3 Jinsi ya tatu

#### 2.6.3.1 Mhusika wa miraba minne

Mhusika wa miraba minne huwa na sifa nyingi. Aidha, sifa hizi zaweza kuwa nzuri na zingine zaweza kuwa mbaya. Wahusika hawa hubadilika. Mara nyingi wahusika hawa wakuu ndio huwa wa miraba minne.

#### 2.6.3.2 Mhusika wa mraba mmoja

Mhusika wa mraba mmoja huwa na sifa moja tu. Hawabadiliki kuanzia mwanzo hadi mwisho. Kwa mfano, ikiwa mhusika huyu ni mwandilifu huendeleza sifa hizi za uadilifu kutoka mwanzo hadi mwisho.

#### 2.6.3.3 Wahusika duara

Hawa ni wahusika wa miraba minne ambao wana desturi ya kubadilika kitabia, kimawazo au kisaikolojia. Hubadilisha misimamo yao kulingana na mazingira.Huathirika na hubadilika na kuwa hivi au vile kila wakati.

#### 2.6.3.4 Wahusika bapa

Msanii huwambuni wahusika wanaolingana moja kwa moja na wazo au sifa fulani. Wahusika hawa wamebuniwa kuzingatia na kutenda matendo yanayooana na sifa walizopewa. Wanashika papo kwa papo bila kubanduka, bila kubadilika hata wakati mazingira au mahusiano yanapobadilika. Wahusika bapa ni wa mraba moja nao hugawika kuwili:

##### 2.6.3.4.1 Wahusika bapa sugu

Wahusika hawa hawabadiliki. Ni sugu katika hali zote za maingiliano yao na wengine. hawatingiziki katika tabia, huwa na msimamo thabiti. Aghalabu hutumiwa kuwasilisha hulka zisizoelekea kuwa za kawaida katika jamii.

##### 2.6.3.4.2 Wahusika bapa kielelezo

Kwa mujibu wa  Njogu na Chemerah (1999) wahusika hawa hawabadiliki kitabia. Licha ya hilo, wamepewa majina ya majazi. Aghalabu hutumiwa na waandishi kutoa mfano wa tabia fulani wanazoshikilia hadi mwisho. Aidha, tabia inayoendelezwa na mhusika huyu ni ile iliyokitwa na mwandishi. Mhusika anatumiwa kama kielelezo cha tabia hiyo.

#### 2.6.3.5 Wahusika shinda

Hawa wako baina ya wahusika duara na bapa. Wana uhai na nguvu zaidi kuliko wahusika bapa. Wanategemea wahusika wa aina zote mbili, na wanapelekwa mbele na mawazo na tabia za hao wengine. Wao huonekana wasiokamilika kwa kuwa hutumiwa kuyakuza mawazo ya wengine badala ya mambo yao wenyewe. Kama kuna masuala yao, wao huyagusia tu bali wahusika wengine ndio huwasaidia kupambanua mawazo yao.

#### 2.6.3.6 Wahusika nguli

Hawa ni wahusika wanaowakilisha maadili ambayo ndiyo aghalabu falsafa ya mwandishi. Mara nyingi nguli huwa ni mhusika mkuu kwani ndiye hutumiwa kotekote ili kusambaza ujumbe wa mwandishi.

#### 2.6.3.7 Mhusika mpinzani

Huyu hubuniwa kimaksuudi na mwandishi kuwa wa kukinzana na msimamo wa mhusika nguli. Yeye huenda kinyume na maadili yanayowakilishwa na mhusika nguli. Mfano mzuri ni Ibilisi katika *Utenzi wa Ayub* ambaye hafurahishwi na matendo mema ya Ayub.

#### 2.6.3.8 Mhusika wa kimapinduzi

Huyu ni mhusika ambaye hutumiwa na mwandishi kuonyesha mapambano baina ya walio mamlakani hasa viongozi wa kiimla na wanaopigania ukombozi. Ni mhusika ambaye huwa na uelewa fika wa hali ya mambo na huwaongoza wengine katika mapambano haya. Wakati mwingi huwa ni mhusika mkuu.

Kwa maoni yetu usawiri huu wa wahusika umetufaa sana katika utafiti huu. Aidha, umetusaidia katika uchambuzi wa wahusika na jinsi walivyosawiriwa katika *Utenzi wa Mwana Hasina na Rashidi Walii*. Pia, umetuwezesha kutoa kategoria mbalimbali za wahusika na uhusika wanaopatika katika utenzi huu.

## 2.7 Matumizi ya lugha

Kulingana na Wamitila (2003) wataalamu wa isimu wemeafikiana kuwa lugha ni mfumo wa sauti nasibu, zinazotumiwa na watu wa jamii fulani wenye utamaduni unaofanana kuwasiliana. Kauli hii ina maana kuwa dhima kuu ya lugha ni mawasiliano. Lugha yaweza kuwa ya ishara, mazungumzo au maandishi. Tuki (2004) inasema kuwa lugha ni mpangilio wa sauti na maneno unaoleta maana ambayo hutumiwa na watu au kundi fulani kwa ajili ya kuwasiliana. Mgullu (1999) akimnukuu Sapir (1921) anasema kuwa lugha ni mfumo ambao mwanadamu hujifunza ili autumie kuwasilisha mawazo, maono na mahitaji. Mfumo huu hutumia ishara ambazo hutokea kwa hiari.

Habwe na Karanja (2004) wanasema kuwa lugha yoyote ile hutumiwa kwa urahisi wa kustaajabisha, na wazaliwa wa lugha fulani wanapokutana na kuzungumza kwa kutumia lugha fulani na kuelezana habari za aina mbalimbali. Kufuatia maelezo ya Habwe na mwenzake, tunapata kufahamu kuwa dhima kuu ya lugha ni mawasiliano.

Kufuatia maelezo ya wanaisimu hawa tunaona kuwa lugha hutumiwa na wanadamu na ilitumiwa tangu awali. Tofauti na lugha ya kawaida itumiwayo na wanajamii, taaluma ya fasihi hutumia lugha ambayo hutofautiana kwa kiasi fulani na lugha ya kawaida. Sifa za matumizi ya lugha zinatokana na sifa za ushairi wenyewe. Waasisi wa nadharia ya Urasimu wa Kirusi wanasisitiza haja ya upekee wa lugha ya kishairi. Wanaeleza kuwa kilichopo si washairi bali ni ushairi. Kama njia ya kusisitiza umuhimu wa matumizi ya lugha ya kishairi Kitula na Amata (2001) wanaeleza kuwa:

> Shairi ni chombo kinachomwezesha mwandishi kufumbata upana wa maisha, katika maneno teule machache yaliyofinyangwa kisanaa. Uteuzi huo wa maneno hupangiliwa kama vito kwenye kazi ya sonara anayefua chombo cha dhahabu. Vito kwenye jicho la mvuaji na mtazamaji, mpangilio wa maneno teule katika ushairi hujenga picha na tashbihi inayojenga maana na mantiki inayochorwa na mashairi lakini nia yake imo katika kukamilisha hisi kwa msomaji au msikizaji kama vile: Hisi za mapenzi, chuki, dhiki, faraja, ari au mapuuza, ujinga au werevu, sifa au tashtiti pamoja na kumzindua.

Wanaendelea kusema yafuatayo:

> Ingawa ushairi ni pambo la lugha na usanifu, mashairi hayawezi kuwa yenye mvuto iwapo hayahusu hisia na mambo yanayowafahamikia wote waishiyo katika jamii inayohusika.

Wamitila (2008) anasisitiza kuwa mchanganuzi wa mashairi anapaswa kujiuliza maswali kadhaa: Je msamiati anaoutumia mtunzi ni msamiati wa kawaida au msamiati maalum? Je, ikiwa msamiati ni mwepesi au mzito ni athari gani inayoachwa na msamiati huo? Je, msamiati huo unaathiri vipi maana ya fasihi katika shairi lenyewe? Je, msamiati huo una umbo la kawaida? Je, yapo maneno maalum ambayo yanaathiri uelewekaji wa shairi linalohusika? Je, maneno yanayotumiwa yana uwezo wa kuibua maana nyingine ya ziada katika shairi? Pamoja na

masuala yanayohusiana na msamiati, mhakiki vile vile anafaa kuchunguza matumizi ya uhuru wa kishairi na tamathali za usemi.

### 2.7.1 Uhuru wa kishairi

Mbatiah (2001) anaeleza uhuru wa kishairi kama dhana ilio na maana mbili zinazohusiana. Kwanza, ni uhuru wa mshairi kukiuka kaida na kanuni za matumizi ya lugha katika viwango vya msamiati, sarufi, sintaksi na kisemantiki. Pili, ni uhuru wa mwandishi wa utanzu wowote wa kukiuka sio tu kaida na kanuni za lugha bali pia kaida za kijamii na kweli za kihistoria. Maelezo haya ya Mbatiah yana dhima kubwa katika utafiti wetu, kwani yanaonyesha kuwa dhana ya uhuru wa kishairi ni pevu zaidi kuliko namna inavyojulikana na kutumiwa na wahakiki wengi wa fasihi ya Kiswahili.

Hata hivyo, katika utafiti wetu kauli ya kwanza ya Mbatiah imetufaa sana katika uhakiki wa *Utenzi wa Mwana Hasina na Rashidi Walii* tulioushughulikia. Aidha, tumechunguza ni vipi malenga anaweza kuboronga sarufi yake na ni kwa nia gani. Mshairi pia ana ule uhuru wa kutumia msamiati wa lahaja mbalimbali. Hali hii haimaanishi kuwa msanii ana uhuru wa kishairi pekee bali pia ana uhuru wa kutumia lugha kwa ujumla wake. Ikiwa kazi yake itasomwa na msomi wa kawaida anaweza kuchukulia huu kama upungufu wa kuimudu lugha lakini kwa msomi wa fasihi atafahamu uhuru alionao mtunzi. Ni muhimu kutaja kuwa wakati mwingine lahaja huenda ikatinga upitishaji wa ujumbe uliokusudiwa, na mtunzi ambapo msomaji anakosa kuelewa maana ya maneno ya kilahaja. Katika utafiti wetu tumechunguza jinsi msanii amefaulu katika matumizi ya uhuru wake ili kufikia malengo yake ya kisanii.

#### 2.7.1.1 Ukiushi wa Kisintaksia

Wamitila (2003) anasema ukiushi wa Kisintaksia ni mpangilio wa maneno katika sentensi, ambapo mtunzi hukiuka miundo ya sentensi iliyozoeleka ya lugha husika katika fasihi ya Kiswahili. Mbinu hii pia hujulikana kama kuboronga sarufi. Mbinu hii pia huchukuliwa kuwa aina ya tabdila kutokana na sababu kuwa huhusisha kubadilisha sarufi ya lugha husika. Kwa mfano: ‘Sana nikanyenyekea’ badala ya ‘nikanyenyekea sana.’ Mtunzi hutumia ukiushi huu wa kisintaksia kwa kusudi la kuleta urari wa vina na pia kuipa kazi yake rithimu pamoja na wizani. Hali hii pia huonyesha kiwango cha usanii cha mtunzi na humpa uwezo wa kuweza kukoleza

kazi yake zaidi kinyume na ambavyo angeitumia lugha ya kawaida. Pia, ukiushi huu humpatia msomi mvuto wa aina fulani kwani unakiuka ukawaida uliozoeleka.

#### 2.7.1.2 Ukiushi wa kisemantki

Wamitila (2003) anasema ukiushi wa kisemantiki ni aina ya uhuru wa kishairi ambao unahusu kuzua kauli ambazo zinaleta maana, ambayo ni mpya kwa kutumia njia isiyo ya kawaida. Kwa mfano, uhuishi unahusu kuvipa vitu sifa za binadamu vitu ambavyo havina uhai. Kwa mfano, katika *Utenzi wa Vita vya Maji Maji,* ubeti wa 151, mtunzi amesema, 'Nyoyo zao zikatapa,' Nyoyo zimepewa sifa za binadamu. Mtunzi hutumia ukiushi huu ili kupatia utunzi wake uhai na kuuhusisha na hali halisi katika jamii.

#### 2.7.1.3 Ukiushi wa kimofolojia

Murage (2011) anaeleza kuwa uhuru wa kimofolojia hutumiwa kueleza aina ya ukiushi katika uendelezaji wa maneno. Kuna ukiuishi wa aina tatu wa kimofolojia: Inkisari, mazida na tabdila.

##### 2.7.1.3.1 Inkisari

Inkisari ni ukiushi katika kiwango cha kimofolojia. Mtunzi hupunguza baadhi ya mizani katika maneno mengine shairini. Lengo kuu huwa ni kupata muumano wa mizani. Malenga huwa na uhuru wa kuyafupisha maneno atakavyo bora yaendelee kuwa na maana ya kawaida.Inkisari hutumiwa mwanzoni au katikati ya neno. Kwa mfano:'lipoingia'badala ya'alipoingia.' Katika neno hili ufupishaji umetokea mwanzo mwa neno. Mfano wa pili; 'semapo wende,' badala ya 'usemapo waende.' Ufupishaji umetokea mwanzoni na katikati mwa neno.

##### 2.7.1.3.2 Mazida

Mazida ni mbinu ya kuongeza mizani katika maneno ya shairi. Lengo lake likuwa ni kutafuta urari ufaao wa idadi ya mizani katika kila kigao au mshororo. Mfano wa mazida unajitokeza katika *Utenzi wa Vita vya Maji Maji* katika ubeti wa 27 ambapo mtunzi ametumia neno 'tukaizua' fitina badala ya 'tukazua' fitina. Sababu ya kufanya hivyo ni kuongeza idadi ya mizani katika mshororo huo na vilevile kupata urari wa vina.

##### 2.7.1.3.3 Tabdila

Tabdila ni mbinu inayotumiwa katika ushairi kubadilisha miundo ya maneno fulani. Kimsingi hutokana na sababu za kiarudhi ili kupata urari wa vina na kuongeza mvuto kwenye lugha.

Mfano wa mbinu ya tabdila katika *Utenzi wa Vita vya Maji Maji*, ni: 'Sirikari' badala 'serikali' katika ubeti wa 10, pia katika ubeti wa 41 ametumia 'swilaha' badala ya 'silaha'.

#### 2.7.1.4 Lahaja

Mwilaria (2011) anasema lahaja ni matumizi ya kilafudhi ambapo maneno hutamkwa kulingana na watamkavyo wakazi wa jamii fulani ziongeazo Kiswahili kisicho sanifu. Watunzi wana mazoea ya kutumia msamiati kutoka kwa lahaja mbalimbali katika utunzi wao. Matumizi ya maneno ya kilahaja huwa mojawapo wa uhuru wa matumizi ya lugha katika kiwango cha kimofolojia. Ifuatayo ni mifano ya lahaja:

##### 2.7.1.4.1 Kingozi

Kingozi kinaaminika kuwa na asili yake katika mji wa kale ulioitwa Ngozi. Lugha yenyewe inajulikana kama Kingozi. Ni lugha ya zamani sana ya pwani na miundo yake hupatikana katika ushairi lakini lugha yenyewe imepotea kwa mujibu wa Mwilaria (2011). Baadhi ya maneno ya kingozi katika *Utenzi wa Masahibu* ni: 'Upulike' badala ya 'usikilize' ubeti wa 29, 'ndwee' badala ya 'ndwele' ubeti 26.

##### 2.7.1.4.2 Kiamu

Kiamu ni mojawapo wa lahaja za kale sana na ambayo inatumika mjini Lamu. Jina Lamu linatokana na Kabila moja la Kiarabu lijulikanalo kama Banu Lami lililotoka Ghuba la Uajemi. Jina la kale sana la Lamu lilikuwa 'Kiwa Ndeo.' Ni lugha iliyotumika sana Lamu na imetumiwa sana katika uandishi wa tenzi za kale. Katika Kiamu, sauti /z/ hutumika badala ya /v/, /t/, /ch/ na /y/ badala ya /j/. Irabu /ee/ zikifuatana konsonanti /l/ huwekwa katikati. Kwa mfano, 'mbee' huwa mbele. Isitoshe konsonanti /l/ na /r/ hudondoshwa zikiwa katikati ya irabu mbili. Mfano; 'Kuea' hubadilika na kuwa 'kulea' ilhali 'chua' hubadilika na kuwa 'chura.' Haya ni kutokana na Mwilaria (2011).

##### 2.7.1.4.3 Kiarabu

Waarabu walikuwa miongoni mwa wageni waliozuru Pwani ya Afrika ya Mashariki. Walikuwa na lengo la kufanya biashara na pia kueneza dini ya Kiislamu. Kufuatia maingiliano yao na wenyenji wa pwani ya Afrika Mashariki, lugha ya Kiswahili ilipata kukopa maneno mengi kutoka kwa lugha ya Kiarabu. Kwa mfano, katika *Utenzi wa Kutawafukwe Mtume Muhammadi* kuna matumizi ya maneno kame vile:

| **Kiarabu** | **Kiswahili** |
|---|---|
| Qalamu | kalamu |
| Kukutubu | kuandika |

### 2.7.1.5 Tamathali za usemi

Tamathali za usemi hujulikana kama lugha ya kitamathali. Kuhenga (1977) anaeleza tamathali za semi kama nguzo za ufasaha na pambo za lugha, na huwezesha mdarisi wa lugha kupakua baadhi ya uhondo uliofichika katika lugha. Maelezo haya yana maana kuwa, tamathali za usemi ni mojawapo ya mbinu za kiubunifu za matumizi ya lugha ya kifasihi. Tamathali za usemi hutumiwa kueleza fungu la maneno, au hata neno ambalo limegeuzwa maana yake ya kiurejelezi na kuwa na maana nyingine. Jambo hili linamaanisha kwamba tamathali za usemi hukiuka matumizi ya lugha katika viwango viwili. Kiwango cha kisemantiki na kile cha kisintaksia.

Ni muhimu kutaja hapa kuwa tamathali za usemi nyingi huwa na mpaka finyu sana kati yazo. Kwa hivyo, ni muhimu msomaji awe na uelewa wa kina ili aweze kupata ujumbe ulionuiwa na mtunzi. Baadhi ya tamathali zilizotumiwa katika fasihi ya Kiswahili ni kama vile: Tashibihi, chuku, sitiari, tashhisi, misemo, kejeli, dhihaka na maswali ya balagha miongoni mwa nyingine. Katika sehemu hii tutaeleza misingi ya uhakiki wa baadhi ya tamathali za usemi. Tamathali tunazojadili ni zile zilizotumika kwa kiwango kikubwa katika *Utenzi wa Mwana Hasina na Rashidi Walii.* Baadhi ya tamathali zilizotumika katika utenzi huu ni pamoja na:

#### 2.7.1.5.1 Sitiari

Tambasi (2011) anasema kuwa sitiari ni mbinu ya kulinganisha vitu ama watu bila kutumia viunganishi linganishi kama vile: Mithili ya, mfano wa, sawa na, na vinginevyo. Kwa hivyo, katika tamathali hii, vitu na watu hulinganishwa na vitu na watu wengine kama kwamba vitu na watu hao ni sawa kabisa. Sitiari hutumika kwa nia ya kulenga hisia za msomaji na pia kujenga picha fulani akilini mwa binadamu ambaye ni msomaji wa kazi ya kifasihi inayohusika. Sitiari humwezesha msomaji kutafakari kuhusu taswira iliyojengeka akilini na kupata ufahamu wa kina wa wazo ambalo msanii ananuia kupasha kwa hadhira yake.

Katika mashairi ya Liongo, sitiari inadhihirika katika ubeti wa kwanza ambapo Liongo anaitwa 'simba' ili kuonyesha nguvu zake:

Nabudi takhamisi kidiriji
Niwathihishe izagale kama siraji
Ili kufuasa yaliongo simba wa miji
Ai wanji wanji naza wanji kisiza wanji na kadiliza
Kasiliza, mwanangwa mema

**2.7.1.5.2 Chuku**

Murage (2011) anasema kuwa chuku ni tamathali inayotia chumvi kuhusu uwezo wa viumbe, tabia zao na kuhusu sifa zao kwa madhumuni ya kuchekesha au kusistiza. Kauli zinazotumika katika mbinu hii huwa ni za kutiliwa chumvi ili kusisitiza na pia kuchekesha. Hali ambayo inamtia msomaji motisha ya kuendelea kuisoma kazi fulani. Pia, huondoa ukinaifu kwa msomaji na kumpa mshawasha wa kuendelea zaidi kusoma kazi husika. Ufuatao ni mfano wa chuku katika *Utenzi wa Siri li Asirali* katika ubeti wa 245:

Kula mumoya rijali
Kwemea mwende hajali
Kukazuka zilizali
Ba'azi yao ba'azi

Ubeti huu unasimulia vita kati ya Shekhe Ali na Azaruni. Mtunzi anatujulisha kuwa kulitokea zilizali. Tunafahamu kuwa katika maisha halisi hatuwezi kuwa na mtetemeko wa ardhi kwa sababu ya vita vya watu wawili. Mtunzi anataka kutufahamisha kuwa vita vilikuwa vikali.

**2.7.1.5.3 Tashbiha**

Tashbiha ni mbinu ya mlinganganisho wa vitu viwili au zaidi wa kutumia maneno kama vile: Mithili ya, kama, kwamba na mengine mengi. Ifuatayo ni mifano ya tashbiha:

Bwana Msa ni mweusi kama makaa.
Urembo wake ulikuwa sawa nawa malaika.

Tashbiha hujenga taswira machoni mwa msomaji na kumsaidia kupata picha kamili kuhusu kinachozungumziwa.

**2.7.1.5.4 Tashihisi**

Tashihisi ni aina nyingine ya tamathali za semi. Kwa tamathali hii vitu visivyo na sifa walizo nazo watu hupewa sifa hizo. Aghalabu sifa hizo za uhai huwa zinalenga kuvitukuza vitu hivyo.

Wamitila (2008) anaeleza kuwa tashihisi inaweza kutazamwa kama aina ya sitiari kwa sababu ya kulinganisha vitu vilivyo hai na visivyo hai. Hata hivyo, ni ya moja kwa moja kinyume na tashihisi ingawa zote zinahusika na uhamishaji wa maana. Ufuatao ni mfano wa tashihisi katika *Utenzi wa Vita vya Maji Maji* ubeti wa 173:

‘hongo tupe maarifa!’
Watu wengi wamekufa
Bara yote inaafa
Wapi kafanye shauri

‘bara yote inaafa’ ni uhuishaji.

**2.7.1.5.5 Takriri**

Murage (2011) anaeleza kuwa tamathali hii inahusu utokeaji wa mara kwa mara au wa kurudiwarudiwa katika matini. Kwa vile urudiaji ni wa aina nyingi, katika utafiti wetu tutatumia dhana ya takriri kama urudiaji unaohusu sauti za lugha. Katika hali hii tunapata urudiaji wa aina tatu wa takriri: Takriri irabu, takriri konsonanti na takriri vina. Takriri irabu inahusu urudiaji wa sauti ya irabu ileile katika neno au maneno ya mshororo mmoja yanayopakana. Urudiaji huu hupatikana katika tungo za kishairi na hudhamiriwa kuleta urari katika shairi.

Takriri vina inahusu urudiaji wa vina, vile vile katika mishororo ya ubeti au shairi lote. Takriri vina ni mojawapo wa kaida muhimu za mashairi ya kimapokeo. Urudiaji wa vina husaidia kuleta wizani katika mashairi. Aidha, takriri konsonanti vilevile hupatikana katika neno au maneno yanayopatikana katika mshororo. Pia, hupatikana katika mianzo ya maneno ya mishororo ya beti zinazopatikana. Urudiaji huu huwa njia ya kudumisha ridhimu na kuonyesha umahiri wa mtunzi katika usanifu wake. Mfano: Katika *Utenzi wa Vita vya Maji Maji*:

Korojo mrojo
Miji wametia fujo
Kumbe povu la mkojo!
Dhalili tena fakiri!

Kiambishi ‘jo’ kimerudiwarudiwa. Takriri huleta msisitizo na hutilia mkazo swala fulani.

#### 2.7.1.5.6 Maswali ya balagha

Maswali ya balagha ni maswali yanayotumiwa na msanii ambayo hayahitaji majibu. Mtunzi hutumia maswali ya balagha kwa lengo la kumfanya msomaji atafakari zaidi kuhusu jambo linalozungumziwa ili alifahamu kwa kina. Kwa mfano, katika *Utenzi wa Vita vya Maji Maji* ubeti wa 167, kuna matumizi ya swali la balagha:

Mwalisema maji haya
Ambaye anatumiya
Risasi inaziwiya;
Kwani kuwa ni asari?

'Kwani kuwa na asari' ni swali la balagha.

#### 2.7.1.5.7 Nidaa

Katika matumizi ya nidaa, mtunzi hutumia alama za hisi katika kazi yake kuonyesha mshangao au msisitizo wa jambo lililosemwa. Nidaa pia hutumika kubebea hisia mbalimbali za wahusika katika kazi za kifasihi kama vile uchungu, furaha, masikitiko na mshangao. Pia, humsaidia msomaji kujihusisha na hisia za mtunzi moja wka moja. Ufuatao ni mfano wa mbinu ya nidaa katika *Utenzi wa Vita vya Maji Maji* ubeti wa 7:

Na sasa mseme kweli!
Wala hapana muhali,
Sababu hamna mali,
Ni nani wenu kubari?

Mshororo wa kwanza, 'Na sasa mseme kweli!' unadhihirisha matumizi ya 'nidaa'.

#### 2.7.1.5.8 Taswira

Senkoro (2011) ameeleza taswira kama mkusanyiko wa picha mbalimbali ziundwazo na maelezo ya wasanii katika kazi za kifasihi. Taswira huambatana na matumizi na tamathali za usemi kama vile sitiari na tashbiha. Taswira ni lugha inayochora picha ya vitu au mahali kwa kutumia ishara.Kwa maoni yetu, taswira ni maneno ambayo hupangwa kisanii katika kazi ya kifasihi, ili yaweze kuchora picha kamili ya kitu au hali katika mawazo ya hadhira.

Senkoro (2011) amegawa taswira katika makundi matatu yakiwemo zionekanazo, za mawazo na za hisi. Taswira zionekanazo ni taswira inayonekana. Mtunzi hupanga matukio mbalimbali ambayo humba taswira zinazooana na kuleta maudhui ya kazi fulani. Taswira ya mawazo ni taswira ambazo ni za kuwazika. Mara nyingi taswira hii husaidia kulifanya fumbo la shairi liwe zito. Taswira hisi ni taswira ambazo huweza kumfanya msomaji au msikilizaji awe na wasiwasi apandwe na hasira, aone woga na kadhalika.

#### 2.7.1.5.9 Kinaya

Mwangi na Wamalwa (2016) wanaeleza kinaya kama matumizi ya meneno yenye ukinzani na anavyodhamiria msemaji. Hapa mwandishi hujenga ukinzani kati ya hali ilivyo na inavyosemekana kuwa.

Kwa maoni yetu kinaya ni mbinu ya msemaji kutoa kauli ambayo ni kinyume na anachomanisha. Kuna aina tatu za kinaya: Cha kiusemi, kinaya cha kihali na kinaya cha kidrama. Kinaya cha Kiusemi ni pale ambapo usemi fulani una maana iliyo kinyume. Aidha, kinaya cha Kihalihuashiria pale matendo ya wahusika yanakuwa kinyume na matarajio ya msomaji. Pamoja na hayo, kinaya cha Kidrama ni pale ambapo kuna matendo au hali fulani ambazo wahusika hawajui kutokea kwake ilihali msomaji anayafahamu.

#### 2.7.1.5.10 Uzungumzinafsia

Uzungumzaji nafsia ni mbinu ambayo mhusika hujizungumzia. Anaweza kuibua mjadala kuhusu jambo fulani na akarudia maneno ambayo yaliyozungumzwa na mtu mwingine akiwa peke yake.

#### 2.7.1.5.11 Methali

Ni semi fupi zinazoeleza kwa muhtasari mawazo au mafunzo ambayo ni mazito na yanayotokana na uzoefu wa jamii. Methali ni semi au kauli zenye busara na mafunzo kuhusu maisha na mahusiano ya watu katika jamii. Methali hutekeleza majukumu anuwai katika jamii. Kwa mfano, huonya, huelimisha, huhimiza au hata kumbeza mtu.

#### 2.7.1.5.12 Misemo

Ni matumizi ya maneno ya kawaida kijozi kwa njia isiyokuwa ya kawaida. Inahitaji msomaji kuwaza ndiposa afichue maana ya maneno husika. Misemo mara nyingi hubuniwa na jamii. Isitoshe, hutofautiana kutoka kwa jamii moja hadi nyingine maanake misemo hutungwa

kutokana na mazingira na itikadi za jamii. Misemo hutumika kwa lengo la kusitiri maana na pia kumfanya msomaji kutafakari ujumbe uliopo. Mifano ya misemo katika *Utenzi wa Vita vya Maji Maji*, 'himahima' kumaanisha haraka na 'hapa na hapa' kumaanisha kila mahali.

**2.8 Usimulizi**

Usimulizi ni uelezaji wa matukio katika hadithi. Wamitila (2003) anaeleza aina mbalimbali za usimulizi nazo ni pamoja na, usimulizi anuawi, usimulizi ngazi, usimulizi maize, usimulizi penyezi, usimulizi sawia, usimulizi tangulizi, usimulizi wa kiutendi, usimulizi wa kirejeshi, usimulizi wa kiutomaji, usimulizi wa nafsi ya kwanza, usimulizi nafsi ya pili na usimulizi nafsi ya tatu.

Mawazo ya Wamitila ni kuwa, kazi zote za fasihi lazima ziwe na matukio na hayo matukio yanaweza kuwasilishwa kwa hadhira kwa njia nyingi za usimulizi. Msimulizi lazima auchague mtindo ambao ni wa kufaa zaidi kuwasilisha mawazo yake yatakayomwathiri msomaji kwa njia moja au nyingine. Usimulizi unaweza kuwa wakufululiza matukio moja kwa moja bila ya kukatiza. Pia, unaweza kuwa usimulizi wa kirejeshi ambapo msimulizi hukatiza mtiririko na kurejelea mambo yaliopita au aweza kukatiza mtiririko wa hadithi na kuweka vifungu kama vile barua. Katika usimulizi wa nafsi ya kwanza, msimulizi aweza kuwa mshirika wa matendo ya hadithi au ashuhudie matendo hayo bila kushiriki. Msimulizi ambaye hashiriki na yuko nje ya hadithi anaweza kueleza hisia na fikra za wahusika wengine na matukio yote ya hadithini. Katika usimulizi wa nafsi ya kwanza kuna mhusika ambaye anashiriki katika hadithi. Yeye huwa anajielezea tu tajiriba zake lakini hana uwezo wa kueleza za mtu mwingine. Msimulizi huyu huweza kujenga uhusiano wa karibu mno kati yake na msomaji. Sisi kama wasomaji tunaona anachoona, kusikia anachosikia na kuhisi anachohisi. Anaposimulia, yeye hutumia viwakilishi 'mimi' na 'ni' vya nafsi ya kwanza.

Usimulizi wa nafsi ya pili huhusisha viwakilishi vya nafsi ya pili 'wewe' na 'u'. Kulingana na Wamitila (2003) aina hii ya usimulizi ni nadra sana kupatikana ingawa kuna mwandishi wa marekani kusini aitwaye Charles Fuentes aliandika riwaya iitwayo 'The Death of Artemio Cruz' akatumia nafsi hii. Usimulizi wa nafsi ya tatu, huwa na matumizi ya 'a' na 'yeye' katika viwakilishi vya nafsi. Ni mtindo ambao hupendelewa sana na wasanii. Hadithi huelezea matukio yanayohusu mtu mwingine msimulizi huwa nje ya hadithi akisimulia juu ya mhusika fulani.

Maoni yetu ni kuwa usimulizi ni utaratibu ambao mtunzi hutumia katika kueleza matukio katika hadithi. Aidha, tunaunga mkono maoni ya Wamitila kuwa usimulizi waweza kuwa wa nafsi ya kwanza, pili na ya tatu.

Walleck na Wallen (1949) wanasema kuwa katika tenzi, mtunzi husimulia kisa kama msimulizi wa nafsi ya tatu. Wakati mwingine huwapa nafasi wahusika wake kuzungumza moja kwa moja. Kuna waandishi ambao huchagua kusimulia kisa pasipo kushiriki moja kwa moja, huwaacha wahusika peke yao na kumruhusu msomaji kumwelewa mwandishi na mitazamo yake kuhusu mambo yanayoikabili jamii.

Welleck na mwenzake wanasema kuwa wahusika katika shairi husemezana. Hii mara nyingi huwa katika mashairi ya malumbano. Usimulizi wa matukio waweza kuwa wa nafsi ya kwanza au nafsi ya tatu. Katika tendi, usimulizi ni muhimu sana kwani huwasilisha ufafanuzi zaidi wa sifa za mandhari,wahusika wake, majukumu yao na matukio yakiwa katika mbinu ya mfululizo au kukatizwa kwa visa. Pia kipengele cha toni hudhihirika katika usimulizi wa msanii.

### 2.9 Hitimisho

Katika sura hii tumeshughulikia mawanda ya uhakiki wa fani. Pamoja na hayo, tumejadili dhana ya fani na kuonyesha vipengele vyake muhimu. Isitoshe, tumejadili vipengele vya fani ambavyo tutavishughulikia katika sura ya tatu, nne na tano. Vipengele vyenyewe ni pamoja na: Msuko, muundo, mandhari, wahusika na matumizi ya lugha. Katika sura ya tatu tutahakiki msuko, muundo, mandhari na pia wahusika katika *Utenzi wa Mwana Hasina na Rashid Walii*.

# SURA YA TATU

# MSUKO, MUUNDO, MANDHARI NA WAHUSIKA

## 3.1 Utangulizi

Katika sura hii tumeshugulikia vipengele vifuatavyo vya fani: Msuko, muundo, mandhari na hatimaye wahusika.

## 3.2 Msuko

Katika sura ya pili, tulieleza msuko kama mfuatano wa matukio katika hadithi kiwakati na kiusababishi. Msuko wa *Utenzi wa Mwana Hasina na Rashidi Walii* ni sahili au msago. Hii ni kwa sababu masimulizi ya utenzi huu yanatiririka kwanzia mwanzo hadi mwisho. Aidha, mtunzi hatumii mbinu rejeshi kwa hivyo hakuna uchangamano katika msuko huu.

*Utenzi wa Mwana Hasina na Rashidi Walii* unahusu hadithi kuhusu Sultani mmoja aliyekuwa na mtoto wa kike pekee. Anampa ushauri mwanaye dhidi ya kujiingiza kwa matendo ya uzinzi kwani kufanya hivyo kungemfedhehesha sana. Hatimaye, anaparamia mapenzi na kujitumbukiza kwenye vitendo vya uzinifu na kuishia katika lindi la maangamizi.

Mtunzi ameanza utenzi kwa kutoa dibaji kwa kutumia mtindo uliozoeleka katika tenzi nyingi. Aidha, ametanguliza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, Mtume Muhammad na aila yake. Hatimaye, anamalizia kwa kuwatakia hadhira kuuwelewa usimulizi wake. Haya ni katika ubeti 1-3.

Katika ubeti wa 4-16, mtunzi anasimulia hadithi kuhusu Sultani mmoja aliyetawala nchi fulani. Anaeleza kuwa alikuwa na mtoto wa kipekee wa kike aliyeitwa Mwana Hasina. Aidha, anamlea mwanawe kwa mapenzi ya dhati na kukidhi mahitaji yote yakiwemo hata kumnunulia vitu vya thamani. Anampa bintiye ushauri dhidi ya kujihusisha na matendo ya uzinzi kwa vile jambo hilo lingewaaibisha wao kama wazazi wake. Anamkubusha fadhila za kimsingi kuwa mtu haitwi muungwana kutokana na aliyemzaa, bali huitwa muungwana kwa tabia zake. Anamtahadharisha dhidi ya kufanya uzinzi.

Katika ubeti wa 17–22 mtunzi anaeleza jinsi Hasina anajitetea kwa babake. Anasema kuwa yeye ni mwandilifu na hawezi kujiingiza kwa uzinzi. Anamhakikishia kuwa hana mwanamume

anayehusiana naye na hatimaye anamwahidi kutoenda kinyume na mawaidha yake. Aidha, Sultani anafurahia na kuzindisha mapenzi kwa mwanaye.

Ahadi za Mwana Hasina zinasahaulika pindi tu, kijana mtanashati aitwaye Rashidi anapojitokeza machoni mwake kama anavyotuarifu msanii katika ubeti wa 22-26. Licha ya kuwa mchochole, alimvutia sana Mwana Hasina. Fauku ya hayo, mtunzi anatualifu kuwa huyu kijana alikuwa ametoka katika aila isiyo na mashiko yoyote.

Rashidi anapoenda barazani kwa Sultani, Hasina akiwa kwa shubaka anamuona na kushikwa na uchu wa mapenzi. Aidha, baada ya baraza kuisha anamtuma Kijakazi ili afanye upekuzi hadi ajue nyumbani kwake. Kijakazi anatii na kufanya kama alivyoamrishwa. Haya ni katika ubeti wa 30:

Kijakazi akambia
Huyule enenda naye
Hata unjue nyumbae
Name nipate ijua

Baada ya upekuzi wa Kijakazi na kugundua mahali Rashidi anamoishi, Kijakazi anamjuza Mwana Hasina. Aidha, Hasina anamwagiza Kijakazi apike chakula kitamu ili siku iliyofuata ampelekee Rashidi. Kesho yake anampelekea na kumpasha ujumbe wa Hasina kuwa angemtembelea jioni ile. Isitoshe, Kijakazi anamuomba asiende popote ili kumngoja mgeni wake. Haya ni katika ubeti wa 31 – 35.

Rashidi anakataa kutumia chakula kile. Hata hivyo, anakubali kumngoja Hasina. Hasina anapofika kwa Rashidi anampasulia barika matakwa yake kwa kumsihi wachumbiane. Aidha, Rashidi anamkubusha kuwa kulingana na desturi mwanamke hapaswi kumfuata mwanamume ila yafaa kuwa kinyume chake. Baadaye, Rashidi anamlazimisha aondoke kwake na kubaki akitafakari suala hilo. Anafanya uamuzi kuzindisha kuomba kwa vile suala hilo lilikuwa hatari kwa imani yake. Haya yanadhihirika katika ubeti wa 36-62. Ufuatao ni mfano wa ubeti wa 62:

Kalala katafakari
Mambo hayo ni haturi
Majira ya ifariji
Kenda Sali na jamaa

Mtunzi anatualifu kuwa, hata baada ya kukataliwa Mwana Hasina anazidisha juhudi za kumpata Rashidi. Anamtuma Kijakazi ampelekee chakula kwa mara ya pili. Rashidi anamkemea sana Kijakazi na kumtuma kwa Hasina amwambie akome kwenda kwake. Mwana Hasina baadaye anafika na kuzidi kumshawishi awe na uhusiano naye. Jambo hili linazidi kumkera Rashidi. Anamkubusha kuhusu masaibu yatakayowapata watenda dhambi katika siku ya kiama. Haya ni kama vile: Kurambwa uso na nyoka mwenye sumu, kuishia kutupwa Jahanamu na hatimaye kusononeka sana kabla ya kutolewa roho. Haya ni kutoka ubeti wa 63 – 102. Ufuatao ni mfano katika ubeti wa 86:

Na mwenye kutenda zani
Atokapo duniani
Ni adhabu kitandani
Kabla ya roho kutwa

Tunaelezwa kuwa wakati huo wote Mwana Hasina alikaa kimya bila kuchangia lakini anaonekana kuchoshwa na yale Rashidi anayoyasema. Hatimaye anamnyamazisha. Anatishia kumfitini kwa baba yake akikosa kuzini naye. Rashidi haogopi vitisho hivi vya Mwana Hasina. Anamjuza kuwa hatabadili msimamo wake. Aidha, anamwamrisha Hasina kuondoka na kumtahadharisha dhidi ya kumtumania chakula, kwa nia ya kumtia dhambini kama inavyodhihirika katika ubeti wa 103 – 111.

Pindi tu Hasina anapofika nyumbani anaangua kilio. Babake anamuuliza kinachomliza. Anadai kuwa hakuwa na Elimu ya Dini. Kwa hivyo, anamuomba babake amtafutie mwalimu wa dini ambaye angemfunza. Aidha, babake anasema kuwa mwalimu mzuri wa dini katika mji ule ni Rashidi kwa vile alikuwa mwandilifu. Pamoja na hayo, Hasina anamsihi Sultani kumnjengea nyumba mbali na mji mahali ambapo hapakuwa na kelele. Anakubali na kuinjenga ile nyumba kwa wiki moja. Baadaye, Sultani anamwita Rashidi na kumwomba amfunze mwanawe Elimu ya Dini ya Kiislamu. Haya ni katika ubeti wa 112 – 135. Rashidi tayari anajua hila zake Hasina na hata ingawa amekubali kumfunza, anabuni mbinu ya kujinusuru kutoka kwake. Aidha, anamuomba Sultani ruhusa akavitafute vitabu vyake alivyodai vilikuwa vimepotea na kwa hivyo, alihitaji muda wa kuvitafuta na kuvikarabati. Haya ni katika ubeti wa 136 - 137.

Mtunzi anatujuza yaliyojili Rashidi alipofika nyumbani kwake. Anachukua kisu na kukata sehemu zake nyeti. Tena anazianika hadi zikakauka kisha anaziweka kwa kifurushi. Aidha, anasubiri hadi apone na hatimaye anampelekea Sultani na kumwomba amwekee hirizi ile. Anamuahidi kuichukua baada ya kukamilisha kumfunza Hasina. Haya ni katika ubeti wa 138 ambapo mtunzi anasema:

Basi akaenda kwake
Kusema na moyo wake
Akatwa kisu chake
Akajihasi akamaa

Sultani hatimaye anampa Rashidi mwanaye na kumsihi amtunze vizuri kwa vile bado ni mtoto mdogo. Anapendekeza asitoke nje na pia asiruhusiwe kujipikia. Sultani anaahidi kugharamia kila kitu wangetumia na kuwaendea baada ya kipindi cha mwaka mmoja.

Mwana Hasina anazidi kumwandama Rashidi. Anamuarifu kuwa yeye hakuwa na haja na Elimu ya Dini. Lengo lake kuu lilikuwa ni kumfanya Rashidi awe mpenziwe. Anamwarifu kuwa kusema ajengewe kando na mji alinuia kudumisha ufaragha ili waweze kuhusiana bila kusumbuliwa. Aidha, anajaribu kumlazimisha wafanye ngono lakini juhudi zake zinagonga mwamba. Anaapa kulipiza kisasi. Mtunzi anasema kuwa anaenda kwa wachunga mbuzi na kufanya mapenzi na mmoja wao. Anafanya hivyo mpaka anatungwa mimba. Isitoshe, anatishia kumsingizia Rashidi kuwa ile mimba ilikuwa yake. Baada ya mwaka mmoja Sultani anawatuma waungwana kumwendea Hasina.

Msanii anaeleza ghadhabu ya Sultani alipomwona mwanawe akiwa mja mzito. Kwa hasira anamwuliza Rashidi yaliyojiri. Rashidi anamwambia aulize bintiye kisha angeelezea baadaye. Ghafla Hasina anaanza kulia na kudai kuwa Rashidi alikosa kufuata maagizo ya Sultani. Kwa hamaki Sultani anamkemea sana Rashidi na kumweka nguzoni ampige fimbo mia kwa vile, hiyo ndio ilikuwa adhabu kwa wazinzi. Rashidi anasihi umati umuulize Sultani anamuadhibia nini ili afahamu. Anapoelezwa anamwomba Sultani kumpa hirizi aliyokuwa amemwachia. Inapoletwa anasema avuliwe nguo ili ukweli ujulikane. Wote wanashangaa baada ya kuona kuwa Rashidi hakuwa na uwezo wa kutunga Hasina mimba. Sultani anamwomba Rashidi msamaha. Aidha, anampa Rashidi mali nyingi lakini anaikataa. Mwishowe Mwana Hasina anasema kuwa ile mimba ilikuwa ya Salim aliyekuwa mchunga mbuzi. Sultani anatumana aletewe na kuchapwa

viboko mia moja wakiwa na Mwana Hasina. Wanachapwa hadi kufa. Haya ni kutoka ubeti wa 167 – 200.

Mtunzi anamalizia usimulizi wake kwa kutufahamisha jina lake. Anasema anaitwa Saidi na babake ni Abdallah. Hatimaye anatujuza kuwa jalali alimtunza Rashidi kwa kumurudishia sehemu zake nyeti. Hayo ni katika ubeti 203 na 204.

Haya hayule Kashidi
Haja zikarudi
Kakudurae walidi
Mama vilevile awa

Kama vilevile awali
Akatimia kamili
Kakudurae jalali
Kwa fadhili yake nia

Kupitia muhtasari huu ni bayana kuwa mtunzi amefuata kaida tulizozitaja hapo mwanzo katika uteuzi wa msuko. Kwanza tumegundua kuwa matukio yanafuatana kiusababishi na kwa njia ya mantiki kutoka mwanzo hadi mwisho. Aidha, tokeo la kwanza linasababisha la pili na la pili kusababisha la tatu. Kwa mfano, tendo la Hasina kukataliwa na Rashidi linambidi amwombe babake kumtafutia mwalimu ambaye angemufundisha Elimu ya Dini. Pia, anamsihi babake amjengee nyumba iliyokuwa mbali na mji. Anafanya haya yote ili kumwingiza Rashidi kwenye mtego. Naye Rashidi anapofahamu angekuwa mwalimu wake wa dini anakata sehemu zake za siri kwa vile alijua hila zake.

### 3.3 Muundo wa nje

Kama tulivyosema katika sura ya pili muundo wa nje wa tenzi unahusu urefu, beti, mishororo, vipande, mizani, vina na kibwagizo. Muundo huu wa nje ni wa muhimu sana kwani ndio huupa ushairi husika sura au umbo la nje.

Muundo wa *Utendi wa Mwana Hasina na Rashidi Walii* umetosheleza kaida za utunzi wa utenzi. Utenzi huu una jumla ya beti 204 na usimulizi umeanza ubeti wa 4 hadi ubeti wa 204. Isitoshe, utenzi huu una mishororo minne katika kila ubeti na kipande kimoja. Hii ni mojawapo ya sifa za utendi.

Tulieleza mizani kama silabi zinazopatikana katika neno na huleta urari na mdundo fulani katika ushairi wa Kiswahili. Kila mshororo wa *Utenzi wa Mwana Hasina na Rashidi Walii* una mizani minane. Ni kaida ya tenzi kuwa na mizani chini ya kumi na miwili na nyingine huwa na mizani 6 kwa kila ubeti. Ufuatao ni mfano wa mizani katika ubeti wa 134:

Le - o - na - ta - ka - ru - hu – sa

Ha - vi - le - ke - ze - vi – ki - sa

Ya - po - ni - me - ya - fu - a ba

Ni – ta – ku - ja – ku – m – twa – a

Idadi ya mizani ni 8 katika *Utenzi wa Mwana Hasina na Rashidi Walii*. Ufuatao ni mfano wa ubeti wa 171:

O - ndo - ka we - ne - nda - we - we
1 2 3 4 5 6 7 8

u - ka - mu - u – za - mwe - nye - we
1 2 3 4 5 6 7 8

a- li – na – yo – u – ya – ju – we
1 2 3 4 5 6 7 8

Na - ya - pa - te - ni - e - le - ze
1 2 3 4 5 6 7 8

Mtunzi amezingatia kanuni ya mizani katika utenzi mzima. Jambo hili linafanya utenzi ukaririke kwa mapigo. Aidha, mtunzi ametumia uhuru wa mshairi katika kutosheleza mizani, kudumisha maana na mahadhi ya utenzi. Mbinu hizi ni kama vile inkisari, tabdila na mazida. Tutazichunguza na kuzitolea maana katika utafiti wetu.

Tulielezea vina kama urudiaji wa sauti za aina moja unaotokea mwishoni mwa mshororo katika kila ubeti katika utenzi. Vina katika *Utenzi wa Mwana Hasina na Rashidi Walii* vinabadilika ubeti hadi mwingine. Hivi ni kumanisha kuwa kila ubeti una urari wake kivina. Mfano ubeti wa 2 na 81.

Wandika na muhamadi
Salai illahu saidi
Ndipo nipate miradi
Nitakayo yaniwiya

Kwamba wataka niseme
Nataka uwe mume
Wala msichi mfalme
Baba aliyenizaa

Huo ni mfano wa urari wa vina kimshororo katika kila ubeti.

Aidha, tumegundua kuwa kina cha kiishio katika takribani beti 171 ni ‘a’. Mfano katika ubeti wa 8, kina cha kiishio ni ‘a’.

Ewe mwangu Hasina
Wasia sikia sana
Ujitahidi na zina
Allan – allan na kwambia

Isitoshe, kina cha kiishio cha beti zinazobaki 29 ni ya au wa. Kwa mfano, kina cha kiishio katika ubeti wa 1 ni ‘wa’ na kina cha kiishio katika ubeti 7 ni ‘ya’

Awali jina la Rabu
Bisimillahi kutubu
Il-Rahamani iribu
Nai Rahimu ukuwa

Huwanja kusoma duwa
Dhambi upate fitiwa
Nawe toka kuzaliwa
Wanena hina mabaya

**3.4 Mandhari**

Katika sura ya pili tulifafanua mandhari kama muktadha wa mahali na kiwakati wa kazi ya kifasihi. Kazi za kifasihi huwa na vielekezi vinavyoelekeza kwenye muktadha huo wa kiwakati na wa mahali. Aidha, hivi vyaweza kuwa: Vitu vya kimaumbile, wahusika, hali na hata matumizi ya lugha.

Mazingira katika *Utenzi wa Mwana Hasina na Rashidi Walii* ni ya kimseto. Hii ni kwa sababu ametumia mandhari ya aina mbalimbali ili kufanikisha kazi yake. Mandhari haya yanajikita sana Uswahilini na Uarabuni licha ya kwamba kuna mengine. Aidha, lugha iliyotumika katika utenzi ni mchanganyiko wa lahaja ya Kiamu na Kingozi na pia kuna msamiati wa Kiarabu. Ifuatayo ni mifano ya lahaja hizi: Kiamu ‘mmoya’ badala ya ‘mmoja’ (ubeti wa 4), Kingozi ‘umpelekele’

badala ya ‘umpelekee’ (ubeti 34) na msamiati wa Kiarabu, ‘katakalamu’ badala ya ‘akasema’(ubeti wa 164).

Aidha, utenzi unapoanza mtunzi anarejelea mandhari ya kinyumbani ambapo Sultani anampa mwanawe malezi mema. Pamoja na hayo, anamshauri awe mwadilifu na kumtahadharisha asijiingize kwa uzinizi. Mandhari haya ni muhimu kwa sababu yanadhihirisha hali ya uwajibikaji wa Sultani kama mzazi kama tunavyoalirifiwa katika ubeti wa 9, anatekeleza majukumu yake ipasavyo.

Tena ni katika mazingira yaya haya ambapo Hasina akiwa juu ya shubaka anamuona Rashidi na kufumwa na mshale wa mapenzi kwake. Rashidi alikuwa amehudhuria baraza katika ubeti wa 29. Pia tunajuzwa baraza lilikuwa nyumbani kwa Sultani babaye Hasina. Aidha, ni katika mazingira haya ambapo Hasina anataka upekuzi ufanywe ili ajue makao yake Rashidi. Ugunduzi huu ni muhimu kwa sababu utamuwezesha kutekeleza lengo lake.

Pia, kuna mandhari ya kijamii. Mandhari haya yanadhihirika tunaposhuhudia mshikamano mkubwa kati ya wanajamii. Kwanza, uhusiano wa Mwana Hasina na Kijakazi unaonyesha usuhuba mkubwa sana kati yao. Aidha, Hasina anapomtamani Rashidi anamtuma kijakazi akampelelezee makazi yake. Tena anamtuma kumpelekea chakula na jumbe zake za kutaka miadi naye. Pamoja na hayo, kila anapomtembelea Rashidi wanaandamana na Kijakazi. Hii ni dhihirisho tosha kuwa hawana siri kati yao kama inavyodhihirika katika ubeti wa 48.

Pia, wakati Mwana Hasina anajiandaa kwenda kupata Elimu ya Dini anasindikizwa na wanajamii kama ubeti wa 148 unavyodhihirisha. Mandhari haya yanadhihirisha umoja katika jamii hii. Mfano katika ubeti wa 148, mtunzi anasema:

> Sultani kawataka
> Mtu wa kumpeleka
> Waungwana wakatoka
> Hasina kandarundia

Kuna mandhari ya kiwakati. *Utenzi wa Mwana Hasina na Rashidi Walii* ni utenzi wa kale. Aidha ulitungwa Uswahilini hususan maeneo ya Visiwa vya Lamu. Isitoshe, mandhari haya yanajitambulisha kutokana na matumizi mengi ya lahaja za Uswahilini kwa vile mashairi ya kisasa hayana maneno mengi ya lahaja. Pia, kuna mandhari ya kidini. Mtunzi anatanguliza utenzi

kwa mtindo uliozoeleka kwa waumini wa dini ya Kiislamu. Aidha, anamsifu Mungu, Mtume Muhammad na mwishowe aila yake Muhammad. Pia, anamwonyesha kijana Rashidi kama hakimu wa sheria katika Dini ya Kiislamu. Anatufahamisha alikuwa mwandilifu na mcha Mungu. Amesawiriwa kama mhusika mtakatifu anayeogopa dhambi na kukiuka sheria za Dini yake ya Kiislamu kama mtunzi anavyotufahamisha katika ubeti wa 25.

Wakati Mwana Hasina anapomwomba babake kumpa Elimu ya Dini Sultani anamjengea mahali pa kujifunzia. Elimu hii inachukuliwa kama msingi imara kwa waumini wa Dini ya Kiislamu. Fauka ya hayo, wakati Sultani anatekeleza adhabu kwa mwana Hasina na Saimu anafuata Kur'ani. Kur'ani ndicho kitabu kitakatifu cha waumini wa Dini ya Kiislamu. Kwa mfano katika ubeti wa 193, mtunzi anasema:

Sultani akanena
Na aje Mwana hasina
Tufuate kuruana
Kauli yale tafaa

Mandhari haya ni muhimu kwa sababu yanaonyesha imani na sheria za Dini ya Kiislamu na vilevile pana uwezekano wa kuasiwa na baadhi ya wanajamii wafuasi wa dini hii.

Aidha, kuna mandhari ya kidhahania ambayo yanadhihirika wakati Rashidi anamfahamisha Kijakazi kuhusu yatakayotokea siku ya kifo cha mja mwenye dhambi. Fauka ya hayo, mtunzi anatujuza kuwa kutakuwa na kulishwa sumu na matunda ya zakum, nyama za mwenye dhambi kukatwakatwa huku akishuhudia kitendo hicho na hatimaye kukaguliwa na nyoka usoni mwake. Haya ni katika ubeti wa 86 ambapo mtunzi anasema:

Ali mato kutazama
Katavyo zake nyama
Hata mida ukikoma
Ya roho kutaka twaa

Mandhari haya ni muhimu kwa vile yanatoa taswira ya imani ya waumini wa Kiislamu kuhusu yatakayonjiri siku ya kiama.

Pia, kuna mandhari ya malishoni. Katika mandhari haya vijana wa kiarabu wanachunga mifugo. Aidha, mandhari haya yamechorwa kama uwanja mzuri wa kuendeleza tabia ya uzinzi ambapo,

tunapata kuwa kwa kutembea hapa mara kadhaa, Mwana Hasina anatungwa mimba na kijana aitwaye Salim.

### 3.5 Wahusika

Katika sura ya pili, tulieleza wahusika kama viumbe wanaopatikana katika kazi yoyote ile ya kifasihi. Katika *Utenzi wa Mwana Hasina na Rashidi Walii* kuna wahusika wa aina mbalimbali. Kwa mfano:

#### 3.5.1 Mwana Hasina

Mwana Hasina ni mhusika mkuu wa mraba mmoja ambaye habadiliki kuanzia mwanzo hadi mwisho. Ni bintiye wa pekee wa Sultani. Mtunzi amemsawiri mhusika huyu kwa njia mbalimbali. Amempa sifa anuwai, sifa hizo ni kama zifuatazo:

Hasina ni mhusika laghai. Anaendeleza uovu kutoka mwanzo wa utenzi hadi mwisho. Anataka kumlazimisha Rashidi kutenda maovu. Anataka kujamiiana naye. Aidha, anamtishia na kupanga kumzingizia maovu ambayo hakuwa ameyatenda, haya ni katika ubeti wa105, 106 na 154 ambapo tunaelezwa kuhusu mpango huu wa Mwana Hasina anaposema kuwa hima angefanya mizungu, na kumfitini Rashidi ili amweke katika fitina hiyo. Vilevile anamualifu kuwa angemchimbia shimo na kumtia humo ndani asiweze kujitoa. Pamoja na hayo, Hasina anapopata mimba kutoka kwa mchunga mbuzi anadai kuwa mimba ni ya Rashidi. Katika ubeti wa 174 na 175, malenga anatualifu kuhusu kisingizio hiki cha Hasina na anavyokitia chuku, ili Rashidi aonekane kuwa mwovu hata zadi. Anadai kuwa Rashidi hakuwa na utu mbali anamlinganisha na myama kwa kitendo hiki anachodai alikuwa amemtendea.

Mwana Hasina amekengeuka. Anapomwona kijana Rashidi kwa mara ya kwanza anamtamani. Fauku ya hayo, anamtuma Kijakazi amfuate ili ajue makazi yake. Baada ya kugundua makazi hayo anamtembelea Rashidi na kumuuliza awe mpenziwe, jambo hili kama mtunzi anavyotujuza kupitia kwa Rashidi ni kinyume na desturi na imani za dini za Kiislamu. Mwanamume ndiye tu huwa na idhini ya kumtongoza mwanamke wala sio kinyume chake.

Babake anapomwonya dhidi ya kushiriki mapenzi nje ya ndoa, anakula yamini na kumhakikishia Sultani kuwa hangethubutu kumletea aibu ala kuli hali. Lakini pindi tu anapomwona kijana

Rashidi akiwa amehudhuria baraza, ahadi hii kwa baba yake anaisahau na kuanza (kummezea mate) kumtamani kimapenzi kiasi kwamba alianza kupotewa na usingizi akimuwaza.

Hasina ni mnafiki. Anajifanya anataka kusoma Uislamu akiwa na nia ya kumpata Rashidi na kufanya mapenzi naye. Katika ubeti wa 118 – 112, Hasina anadai kuwa yeye ni mwanadamu tena ni Mwisilamu ila hakuwa na ujuzi wa sheria wala Elimu ya Dini, iliyokuwa inawafunza vijana maandili kama vile kutoshiriki kimapenzi nje ya ndoa. Aidha, anamwomba babake amtafutie mwalimu wa dini aliyekuwa mwandilifu ili amfunze mambo hayo ya dini. Fauka ya hayo, Sultani anakubali pendekezo hili la mwanawe bila kujua kuwa, huu ulikuwa ni mpango wa Mwana Hasina wakumnasa Rashidi aliyekuwa tayari amemtamani kimapenzi.

Ni mwenye hila. Alijua vizuri kuwa mwalimu ambaye babake angemtafutia wa dini ni Rashidi na ila si mwingine. Kwa hivyo, anapomsihi babake ampe Elimu ya Dini, babake anamwendea Rashidi na kumwomba amfunze Mwana Hasina. Hii ni kwa sababu katika ubeti 25 Sultani anasema mwalimu aliyeandilika katika mji ule alikuwa si mwingine ila Rashidi.

Mwana Hasina ni mtu asiyekata tamaa. Nia yake ilikuwa kujaribu kumwingiza Rashidi katika mtego wa kufanya mapenzi naye. Alitumia mbinu zote ambazo hazikufua dafu. Kwa mfano, alimtuma Kijakazi akajue anakoishi Rashidi, alimwamuru kijakazi ampikie chakula kisha ampelekee, anajipeleka mwenyewe kwake, anamrarai na kumbembeja, anamtisha Rashidi kwamba atamfitini kwa babake, anajifanya anataka kusoma ili apewe Rashidi kama mwalimu wake na isitoshe anatafuta mimba kwa mchungaji kwa udi na ambari kisha kumsingizia Rashidi mimba hiyo.

Aidha, ni mlipizaji kisasi. Haya yanabainika wakati anapokataliwa na Rashidi. Mtunzi anatualifu kuwa Hasina aliapa kulipiza kisasi. Aidha, tunamuona akienda kwa mchunga mbuzi na kutungwa mimba. Hatimaye, anamsingizia Rashidi kuwa ile mimba ilikuwa yake, ndio maafa ya kutungisha mimba yampate. Aidha, Hasina ni muasherati. Anamtafuta Rashidi akiwa na mpango wa kufanya mapenzi naye. Mpango huu wake unapotibuka, anatafuta njia badala ya kutimiza lengo lake. Aidha, anamfuata mchunga mbuzi ambaye si mume wake halali na kufanya mapenzi naye ambapo anaibukia kutunga mimba.

Pamoja na hayo, Hasina ni msaliti. Anamsaliti babake kwa kufanya mapenzi nje ya ndoa, jambo linalomtia babake aibu kubwa. Tunajuzwa katika ubeti wa 163 alizini na mchunga mbuzi hadi

akapata mimba. Aidha, ni mjanja. Kila alipotaka kutimiziwa haja zake na baba yake alianza kwa kulia kwa simanzi. Juhudi zake za mwanzoni za kutaka kufanya ngono na Rashidi ziliposhindwa kuzaa matunda, alirudi nyumbani akiwa na hasira nyingi na alipofika alianza kulia. Baba yake aliposikia kilio cha mwanaye alitaka kujua kilichojiri. Hazina anamdanganya kuwa alitaka kupata Elimu ya Dini. Mara ya pili tunampata Hasina akilia ni pale anapojengewa nyumba na baba yake mbali na mji na kupatiwa Rashidi kuwa mwalimu wake. Akiwa hapa anaendeleza juhudi zake za kutaka kufanya ngono na Rashidi lakini zinashindwa. Hasina anatafuta mchungaji ambaye anamwendea na kufanya mapenzi naye tena na tena mpaka anapotunga mimba. Baada ya mwaka mmoja walirudi nyumbani. Hatimaye, anamsingizia Rashidi kuwa ile mimba ilikuwa yake.

Zaidi ya hayo, Hasina ni mwenye hasira. Rashidi alipokataa katakata kuingia katika mtego wake, alipiga mayowe na kurarua nguo zake. Jambo hili linamkera sana kiasi kuwa anaapa kulipiza kisasi. Isitoshe, Hasina ni msiri. Anafanya mipango yake ya kutaka kufanya ngono na Rashidi kisirisiri. Hataki baba yake ajue anachopanga. Anaandamana na kijakazi wake kwenda kwa Rashidi wakati wa usiku.

#### 3.5.1.1 Umuhimu wake

Hasina ametumiwa kuonyesha kuwa mchimba kisima huingia mwenyewe. Alimpangia Rashidi maovu lakini maovu yayo hayo yanamkumba yeye. Anadhihirisha kuwa njia ya mwongo ni fupi na kwa hivyo, anatuonyesha umuhimu wa kuwa waaminifu na wakweli kila mara. Anafanya mipango yake kisirisiri lakini uovu wake unagunduliwa baada ya muda mfupi. Pia, ametumiwa na malenga kuendeleza masuala muhimu kama vile nafasi ya mwanamke, ukosefu wa utu, uasherati na unafiki. Kupitia kwake tunaelezwa madhara ya uasherati, kupuuza wosia na kukosa maadili.

### 3.5.2 Rashidi

Ni mhusika mkuu nguli ambaye ni wa mraba mmoja. Kijana wa umri mdogo anayetoka katika familia maskini. Tunampata mtunzi akimtunukia sifa za uongofu si haba. Amempa sifa zifuatazo: Rashidi ni mwenye msimamo thabiti. Alikataa katakata kushawishika kufanya mapenzi na Hasina, licha ya yeye kumrarai na kumbembeja kwa kumpa kijakazi wake chakula ampelekee na baadaye kumpa vitisho vya kuuawa.

Rashidi ni mcha Mungu. Alishinda msikitini akisali na kila mara huenda barazani kuonyesha heshima zake. Hutubu dhambi zake. Anaogopa kutenda dhambi mbele ya Rabana. Anafahamu kuwa siku ya kiyama i karibu, siku ambayo kila mwanadamu atahukumiwa kulingana na matendo yake. Anamwuogopa Mungu. Anafahamu Dini ya Kiisilamu barabara na zaidi ya hayo anaelewa mabaya yote yatakayowakumba wadhambi kama vile kulishwa sumu na matunda ya zakum, nyama za mdhambi kukatwa akitazama, kukaguliwa usoni na nyoka. Mwili kunuka na kuchomwa kwa moto.

Ni mkakamavu. Anachukua kisu na kukata sehemu zake za siri. Anafanya hivi ili kujikinga kutokana na masaibu ya Mwana Hasina, ambaye anajaribu kwa udi na ambari ili wahusiane kimapenzi. Pia, katika ubeti wa 81, Mwana Hasina anapojaribu kumsihi Rashidi wawe na uhusiano wa kimapenzi pasipo kumwogopa babake, Rashidi anasimama kidete na kutetea uamuzi wake. Aidha, anasema kuwa yeye hamuogopi binadamu ila amwogopaye ni Mungu tu. Zaidi ya hayo, anamkemea vikali Mwana Hasina na kumtahadhalisha dhidi ya kujihusisha na matendo yenye dhambi. Anafanya haya kwa kumwalifu kuhusu yale yatakayo mpata adinasi mwenye dhambi. Haya ni katika ubeti wa 107 - 138 .

Ni mdanganyifu. Anamdanganya Sultani kuwa vitabu vyake vya kufundishia vilikuwa vimeraruka. Aidha, anaomba muda wa kwenda kuvikarabati akiwa na nia ya kuutumia muda huo kukata sehemu nyeti na kuzikausha. Anamdanganya Sultani kuwa anampa hirizi amhifadhie mpaka atakaporudi. Pia, anasema kuwa ana mafua kwani hataki kusumbuliwa na Mwana Hasina.

Ni mtiifu.Anakubali kumfunza Hasina Elimu ya Dini ya Kiislamu. Kijakazi wa Hasina anapomwambia atulie nyumbani amngoje Hasina anatii. Zaidi ya hayo, pia alitii mafunzo ya dini kwa kufahamu kuwa kushiriki ngono nje ya ndoa ni dhambi mbele ya Maulana. Aidha, Rashidi ni maskini. Babake hajulikani pia, kabila yao ni duni na hakuna aliyemtambua.

Zaidi ya hayo, ni mwenye hasira. Mlango unapobishwa anauliza kwa hasira kutaka kujua aliyekuwa akibisha. Pia, Mwana Hasina anapomwendea mara kwa mara akitafuta uhusiano wake naye, anaghadhabika na kumulazimisha kuondoka. Pamoja na hayo, ni mshirikina kwani anampelekea Sultani sehemu nyeti na kumweleza kuwa ni hirizi. Pia, ni mwenye itikadi kali. Pindi anapojuzwa na Sultani kuwa angekuwa mwalimu wake Hasina, mtunzi anatufahamisha kuwa aliomba kupewa muda ili aende akavikarabati vitabu vyake baadaye tunaelezwa kuwa,

lengo lake lilikuwa ni kwenda kuzikata sehemu zake nyeti kwa vile alizijua hila za Mwana Hasina.

Rashidi ni mwadilifu. Anafuata maadili na mafunzo ya Dini ya Kiislamu na diposa amejitenga, na vitendo vyote viovu ambavyo vingemwingiza katika dhambi. Maadili ndio yanayomfanya kujitenga na utongozaji wa Hasina. Aidha, ni mtu asiye na uchu wa mali. Sultani anapogundua kuwa Rashidi hakuwa na hatia anataka kumzawadi kwa kumkosea.

**3.5.2.1 Umuhimu wa Rashidi**

Rashidi ametumiwa na mwandishi kuendeleza masuala mbalimbali kama vile uadilifu, umaskini na utabaka. Anaonyesha kuwa wema hushinda uovu. Mwana Hasina anapomsingizia Rashidi kumtungisha mimba na kumfitini kwa baba yake akiwa na lengo la kuuawa kwake, yeye ndiye anayepatikana na hatia na hatimaye kuuawa. Zaidi ya hayo, mwandishi anatudhihirishia kuwa wema hauozi.Rashidi alikataa kutenda maovu alijikata sehemu nyeti ili kujiepusha kutenda dhambi. Mungu alimruzuku baadaye kwa kumrudishia sehemu zake nyeti kiasi kilekile cha awali.

**3.5.3 Sultani**

Sultani ni kiongozi wa nchi fulani. Ana mtoto mmoja tu ambaye ni Mwana Hasina. Ni mhusika wa mraba mmoja. Hakufanikiwa kuzaa mtoto wa kiume. Yeye ni mwenye mapenzi ya dhati. Anampenda bintiye kwa moyo wa dhati. Anampa nguo nyingi, dashidashi na vikuku vya thamani.

Tena ni mshauri mwema. Anampa mwana Hasina mawaidha ya kumwongoza maishani. Anamwambia ajiepushe na dhambi na asiwe na tabia ya kufuatafuata wanaume. Anamweleza kuwa mtu hawi muungwana kwa kuzaliwa na fulani wa fulani na kuwa jina la mtu hutukuka kwa kuwa na unyenyekevu, tena alimwonya dhidi ya kushiriki mapenzi nje ya ndoa. Aidha, ni myenyekevu. Alipogundua kuwa alikuwa amemtuhumu Rashidi bure bilashi anatuma watumishi wake kumwombea msamaha.

Isitoshe, ni mzazi aliyewajibika. Alimlea na kumtunza vyema mwana Hasina. Anamkidhia mahitaji yote na kumpa mawaidha ya kumwongoza maishani. Mwana Hasina anapomweleza

kuwa anataka kuelimishwa Uislamu anajitoa mhanga na kumjengea nyumba nje ya mji na anamwomba Rashidi kuwa mwalimu wake wa dini.

Sultani ni mtu mwenye kujali. Kila mara anapomsikia mwana Hasina akilia anataka kujua kinachomliza. Aidha, ni mwenye hasira. Hasina anapomweleza kuwa mimba ni ya Rashidi anashikwa na ghadhabu kubwa. Anatoa amri atiwe nguzoni na achapwe viboko mia moja.

Sultani ni mzingativu wa sheria. Anatoa amri ya kuuawa kwa Mchungaji na Hasina kwani alitaka kufuata maagizo ya Kur'ani kikamilifu. Pamoja na hayo, ni mcha Mungu. Anachukia dhambi. Anamshauri Mwana Hasina ajiepushe na Ibilisi. Mchungaji na Hasina wanapotenda kinyume na sheria wanaadhibiwa.

#### 3.5.3.1 Umuhimu wa Sultani

Sultani ni kielelezo cha wazazi waliowajibika na walio na mapenzi kwa watoto wao. Anampenda Mwana Hasina na kumkidhia mahitaji yake yote. Alimshauri asiwe na mahusiano na wanaume wengi na kila mara alipomwona bintiye katika hali ya majonzi alikuwa anamtuliza. Aidha, Sultani ametumiwa kuendeleza masuala mbalimbali kama vile utabaka. Yeye ni kiwakilishi cha watu wa tabaka la juu pia anaendeleza maudhui ya mapenzi.

### 3.5.4 Kijakazi

Kijakazi ni mtumishi anayefanya kazi nyumbani kwa Sultani. Ni mhusika mjenzi. Aidha, Kijakazi huyu ni mtiifu. Anapotumwa na Hasina alitumika. Alipoambiwa na Hasina amfuate Rashidi akajue anakoishi, apike chakula na ampelekee Kijakazi alitii.

Kijakazi ni mdanganyifu. Anamweleza Rashidi kuwa Hasina hajaweza kupata lepe la usingizi tangu amwone juzi barazani. Pamoja na hayo, ni mdadisi. Rashidi anapomweleza kuwa hajatenda dhambi tangu kuzaliwa kwake, anataka kujua ni kwa nini basi Rashidi huenda msikitini kufanya dua ili asamehewe.

#### 3.5.4.1 Umuhimu

Kijakazi ni kielelezo cha watumishi wa nyumbani ambao ni watiifu na waaminifu kwa waajiri wao. Kijakazi pia ametumiwa kuendeleza maudhui ya umaskini na utabaka. Anawakilisha watu wa tabaka la chini.

### 3.5.5 Mchungaji/Saimu

Saimu ni kijana Mwaarabu anayechunga mbuzi. Ni mhusika mjenzi. Amepotoka kwa vile anakubali kufanya mapenzi na Hasina ambaye si mke wake halali wa ndoa. Ni maskini hohehahe anayefanya kazi duni ya kuchunga mbuzi.

#### 3.5.5.1 Umuhimu

Kielelezo cha vijana waliopotoka kimaadili na wasioweza kudhibiti hisia zao, kiasi cha kushiriki mapenzi na yeyote wanayekumbana naye. Aidha, Saimu ametumiwa kuendeleza maudhui ya umaskini na utabaka. Anafanya kazi duni naye ni kiwakilishi cha watu wa tabaka la chini.

## 3.6 Hitimisho

Sura hii imehusu uhakiki wa msuko, muundo, mandhari na wahusika katika *Utenzi wa Mwana Hasina na Rashidi Walii.* Msuko wa utenzi huu ni sahili. Muundo wa utenzi huu umefuata kaida za utunzi wa tenzi. Fauka ya hayo, mtunzi amefaulu kubanisha muundo na msuko. Aidha, kuna mandhari mseto katika *Utenzi wa Mwana Hasina na Rashidi Walii*. Pamoja na hayo, utenzi huu una wahusika wa aina mbalimbali: Wakuu, wajenzi, wasasidizi na wadogo ambao wamesawiriwa kwa namna tofauti tofauti. Wametumiwa kuwasilisha dhamira ya mtunzi.

## SURA YA NNE

## MATUMIZI YA LUGHA NA USIMULIZI

### 4.1 Utangulizi

Katika sura ya tatu tulihakiki msuko, muundo, mandhari na wahusika na uhusika. Sura hii imeshughulikia matumizi ya lugha katika *Utenzi wa Mwana Hasina na Rashidi Walii*. Tumehakiki matumizi ya lugha katika viwango viwili: Uhuru wa kishairi na tamathali za usemi. Aidha, tumeshughulikia pia kipengele cha usimulizi. Pamoja na hayo, tumetoa mifano mbalimbali katika *Utenzi wa Mwana Hasina na Rashidi Walii*.

### 4.2 Uhuru wa kishairi

Tulieleza uhuru wa kishairi kama uhuru wa malenga kukiuka kaida za matumizi ya lugha. Katika sehemu hii tunajadili uhuru wa kishairi wa kimsingi uliotumiwa katika *Utenzi wa Mwana Hasina na Rashidi Walii*.

#### 4.2.1 Ukiushi wa kimofolojia

Ukiushi wa kimofolojia katika ushairi ni aina ya uhuru ambapo mshairi anaruhusiwa kuyaendeleza maneno tofauti na jinsi yalivyozoeleka katika lugha sanifu. Malenga ana uhuru wa kuyafupisha maneno, kuyarefusha au kuyapangua na kubadilisha muundo wake. Katika *Utenzi wa Mwana Hasina na Rashidi Walii,* uhuru huu wa mtunzi umedhihirika kwa njia mbalimbali, njia hizi zinajumlisha zifuatazo: inkisari, mazida na tabdila.

##### 4.2.1.1 Inkisari

Katika mbinu ya inkisari, neno huwasilishwa kwa mkato ili kutimiza idadi ya mizani katika mshororo. Maneno yaliyofupishwa katika *Utenzi wa Mwana Hasina na Rashidi Walii* ni kama vile: 'aketa' badala ya 'akamwita' (ubeti wa 6), 'kampa' badala ya 'akampa' (ubeti wa 7), 'atakayo' badala ya  'anayotaka' (ubeti 9), 'apitayo' badala ya 'anayopita' (ubeti 9), 'rohoye' badala ya 'roho yake' (ubeti 12), 'Bilisi' badala ya 'ibilisi' (ubeti 12), 'ushikapo' badala ya 'unaposhika' (ubeti 14), ' atokapi' badala ya 'atokawapi' (ubeti 16), 'nipitepi' badala ya 'nipite wapi' (ubeti 16), 'mfanyia' badala ya 'kumfanyia' (ubeti 16), 'ikisha' badala ya 'ikaisha' (ubeti 26), 'kenda' badala ya 'akaenda' (ubeti 26), 'injua' badala ya 'alipoinjua' (ubeti 33), 'atakayo' badala ya 'anayotaka' (ubeti 43), 'aishiye' badala ya 'anayeishi' (ubeti 103), 'tukutia' badala ya 'nitakutia'(ubeti 105), 'tama' badala ya 'tamaa' (ubeti 109), 'sije' badala ya 'usije' (ubeti 111),

‘kafanye’ badala ya ‘akafanye’ (ubeti 111), ‘asomatata’ badala ya ‘asiye na matata’ (ubeti 119), ‘aso’ badala ya ‘asiye’(ubeti 122), ‘kajibu’ badala ya ‘akajibu’ (ubeti 123), ‘taingiwa’ badala ya ‘nitaingiwa’ (ubeti 126), ‘weka’ badala ya ‘kuweka’ (ubeti 142), ‘kandama’ badala ya ‘kuiandama’ (ubeti 148), ‘shahadayo’ badala ya ‘shahada yako’ (ubeti 154) na ‘wakenda’ badala ya ‘wakaenda’ (ubeti 184). Mifano hii inadhihirisha kuwepo kwa wingi wa inkisari katika utenzi wa *Mwana Hasina na Rashidi Walii*. Kama tulivyoeleza, jukumu kuu la inkisari katika utendi huu ni kutosheleza idadi ya mizani.

#### 4.2.1.2 Mazida

Katika mbinu ya mazida, silabi huongezwa katika neno ili kupata idadi ya mizani inayotakikana na kupata kina kinachofaa. Abedi (1954), anasema ni kuzidisha mizani. Kwa hivyo ni kinyume cha inkisari. Hata hivyo, ametoa tahadhari dhidi ya anayetumia mbinu hii na kuhimiza kuwa lazima anayeitumia asibadili makusudi yanayotakiwa. Mtunzi katika *Utenzi wa Mwana Hasina na Rashidi Walii* amefanikiwa kutoa ujumbe aliyonuia na pia amezingatia idadi ya mizani inayotakikana kwa kutumia mbinu hii. Ufuatao ni mfano wa mazida katika utenzi huu: ‘muuwili’ badala ya ‘mwili’ (ubeti 90), ‘shaitani’ badala ya ‘shetani’ (ubeti 98), mwanaadamu badala ya mwanadamu (ubeti wa 176), muwili badala ya mwili (ubeti 92), (tabdila) na ‘enedeni’ badala ya ‘nendeni’ (ubeti 186).

#### 4.2.1.3 Tabdila

Katika sura ya tatu, tulieleza tabdila kama mbinu inayotumiwa kubadilisha maendelezo fulani. Mtunzi wa *Utenzi wa Mwana Hasina na Rashidi Walii* ametumia mbinu hii, kubadilisha tahajia za maneno bila kupunguza wala kuzidisha mizani kwa lengo la kupata vina. Ifuatayo ni mifano katika utenzi: ‘ifariji’ badala ‘alfajiri’ (ubeti 62), ‘penyi’ badala ya ‘penye’ (ubeti 67), ‘nisikia’ badala ya ‘nasikie’ (ubeti 69), ‘hisabu’ badala ya ‘hesabu’ (ubeti 74), ‘mida’ badala ya ‘muda’ (ubeti 88). Aidha, ametumia wazao badala ya wanao (ubeti 102), labuda badala ya labda (ubeti wa 113), mahala badala ya mahali (ubeti wa 114), ‘ilimu’ badala ya ‘elimu’ (ubeti 115), ‘mumo’ badala ya ‘humo’ (ubeti 154), mtana badala ya mchana (ubeti 161). Pamoja na hayo, ametumia fullani badala ya fulani (ubeti 11), na ndia badala ya njia. Hali hii ya kubadilisha mwendelezo ya maneno huwa na jukumu la kuvutia makini ya hadhira. Pia, mabadiliko hayo ni sehemu ya sajili ya ushairi.

### 4.2.2 Ukiushi wa kimsamiati

Ukiushi wa kimsamiati ni aina ya uhuru wa kishairi ambao unahusu matumizi ya maneno au misamiati mbalimbali ambayo si kawaida kutumika katika lugha sanifu. Ukiushi huu unaweza kutokea katika ukopaji wa msamiati, matumizi ya lugha chakavu na maneno kutoka lahaja nyingine kama vile:

#### 4.2.2.1 Lahaja ya kiamu

Matumizi ya msamiati wa lahaja ya kiamu kama vile alivyotumia mtunzi yanajitokeza katika miundo ifuatayo: /y/ badala ya /j/, sauti /t/ badala ya /ch/ na /d/ badala ya /z/. Kwa mfano, ‘mmoya’ badala ya ‘mmoja’ (ubeti 4), ‘ndiya’ badala ‘njia’ (ubeti 18), na mtukue badala ya mchukue (ubeti 130). Aidha, mtunzi ametumia ‘mtana’ badala ya ‘mchana’(ubeti 54), ‘mwandiyo’ badala ya ‘mwenzio’ (ubeti 154), na ‘mtoe’ badala ya ‘mjue’ (ubeti 151). Zaidi ya hayo, ametumia ‘pamoya’ badala ya ‘pamoja’, ‘hatiya’ badala ya ‘hatia’ (ubeti 190), na ‘nda’ badala ya ‘nia’ (ubeti 193).

#### 4.2.2.2 Lahaja ya Kingozi

Msanii ametumia lahaja ya Kingozi, kwa mfano, ametumia: ‘nikamile’ badala ya ‘nimekamilisha’ (ubeti 3), ‘jinale’ badala ya ‘jina lake’(ubeti wa 23), ‘huyule’ badala ya ‘yule’ (ubeti 27), ‘umpelekele’ badala ya ‘umpelekee’ (ubeti 34), ‘ujale’ badala ya ‘ulija’a (ubeti 1), ‘nijile’ badala ‘nimekuja’ (ubeti 54), ‘wangile’ badala ya ‘waingia’ (ubeti 99), na ‘dondale’ badala ya ‘kindonda’ (ubeti 139). Pamoja na hayo, ametumia ‘mumule’ badala ya ‘humo’ (ubeti 149), ‘jinginele’ badala ya ‘jingine’ (ubeti 176) na ‘mwanale’ badala ya ‘mwana’ (ubeti 180).

#### 4.2.2.3 Msamiati wa Kiarabu

Mtunzi pia ametumia msamiati wa Kiarabu, kwa mfano: ‘Bismillahi’ badala ya ‘Naanza kwa jina la Mwenyezi Mungu’ (ubeti 1). ‘Yurub’ badala ya ‘Mungu’ (ubeti 108), ‘Radidi’ badala ya ‘kurudia’ (ubeti 186), ‘kutakalamu’ badala ya ‘akasema’ (ubeti 164), na ‘Rahimu’ badala ya ‘mwenye huruma’.

Mtunzi ametumia lahaja mbalimbali na msamiati wa kiarabu kuleta mvuto zaidi kwa kazi yake. Aidha, matumizi haya ya lahaja yameashiria usuli wa mtunzi mwenyewe. Pia, yamechangia pakubwa katika ujenzi wa mandhari.

### 4.2.3 Ukiushi wa kisintaksia

Ukiushi wa kisintaksia unajitokeza katika *Utenzi wa Mwana Hasina na Rashidi Walii* pale ambapo, mtunzi amekosa kufuata kaida za miundo ya sentensi kama vile: vishazi na virai kwa mujibu wa kaida za lugha husika. Aidha, uhuru wa kishairi hujulikana kama kuboronga sarufi au mpinduo wa sintaksia. Baadhi ya sehemu hizi ni kama vile ubeti wa 31 mtunzi anaposema:

Akutaka mwonane
Aliyo nayo anene
Wala sifanye mangine
Ya neno lisilo ndia

Katika ubeti huu ametumia 'aliyo nayo anene' badala ya anene aliyo nayo. Mifano zaida ni kama ifuatayo:

| Mifano ya kuboronga sarufi | muundo halisia | ubeti |
|---|---|---|
| Dhabi pata futiwa | upate futiwa dhabi | 71 |
| Kesho kwenda adhibiwa | kwenda adhibiwa kesho | 71 |
| Hajui yangu miradi | hujui miradi yangu | 78 |
| Kesho kwenda kutiwa pingu | kwenda kutiwa pingu kesho | 83 |
| Roho kutaka twaa | kutaka kutoa roho | 88 |
| Mwana akamwendea | akamwendea mwana | 115 |
| Binti yangu pokea | pokea binti yangu | 129 |
| Siku nyingi wakaketi | wakaketi siku nyingi | 22 |

Ukiushi huu ni muhimu sana kwa vile humpa msomaji mvuto wa aina yake, kwani unakiuka ukawaida uliozoeleka. Pia, mtunzi ametumia ukiushi huu kwa kusudi la kuleta urari wa vina na pia kupa kazi yake rithimu pamoja na wizani.

## 4.3 Tamathali za usemi

Katika sura ya pili, tulisema tamathali za semi ni fungu la maneno ambalo limegeuzwa maana ya kiurejelezi na kuwa na maana nyingine. Ifuatayo ni mifano ya tamathali za semi:

### 4.3.1 Maswali ya balagha

Maswali ya balagha ni maswali ambayo majibu huwa wazi kwa hivyo hayahitaji majibu. Katika *Utenzi wa Mwana Hasina na Rashidi Walii,* mtunzi ametumia maswali ya balagha kwa kiasi

kidogo sana. Nia yake ikiwa ni kumtaka msomaji aweze kutafakari zaidi juu ya wazo fulani. Ufuatao ni mfano katika ubeti wa 18:

Mtu huyu atokapi?
Au apite kwa wapi?
Hata nipitepi?
Hata nikapata ndia

Haya yanasemwa na Hasina katika juhudi za kumhakikishia babake kuwa hawezi kujiingiza kwa uzinzi.

**4.3.2 Tashbihi**

Tashbihi ni usemi wa kufananisha vitu viwili visivyo fanana, kwa kutumia maneno kama vile: kama, ja, mfano wa, na mithili ya. Mfano huu huweza kuwa wa: kitabia, rangi na kimaumbile. Picha anayochora msanii huwa na athari kubwa kwa hadhira. Katika utafiti huu tumechunguza jinsi mtunzi wa *Mwana Hasina na Rashidi Walii* amewasilisha ujumbe wake kwa kutumia tashbiha. Aidha, katika ubeti wa 91, mshororo wa pili mtunzi amesema:

Ni harufuyo dhaifu
Yanuka jayama mfu
Wala siwezi isifu
Harafu kwa kwambia

Neno jayama ni sawa na neno kama. Hii tashbihi inalinganisha harufu ya adinasi mwenye dhambi na ile ya mfu. Mtunzi amedhamiria kutupa taswira yatakayotokea siku ya kifo cha binadamu mwenye dhambi. Wafuasi wa dini ya Kiislamu wanaamini kuwa mwili wa mwenye dhambi lazima utatoa harufu mbaya.

Mtunzi anazidi kueleza kuhusu mja aliye mzinzi. Anasema kuwa baada ya kifo chake, nyoka ataukagua uso wake. Aidha, atamsomea na kumkenjeli na kuifananisha harufu itakayotoka kwa mwili wake na ile ya mbuyu na fitida. Haya yanadhihirika katika ubeti wa 96 mtunzi anaposema:

Leo wanuka uvudo
Kama mbuyu na fitido
Punde wamena kishindo
Munkari kamuawia

‘Kama mbuyu na fitindo’ndio tashbihi.

#### 4.3.3 Takriri

Takriri ni mbinu ya kurudia irabu, konsonanti au silabi au neno. Katika utungo wa utenzi wa *Mwana Hasina na Rashidi Walii*, mtunzi ametumia mbinu hii kwa kina. Aidha, ametumia takriri irabu, takriri konsonanti na takriri neno.

##### 4.3.3.1 Takriri irabu

Takriri irabu inahusu kurudia irabu ile katika sehemu sawia za neno katika sentensi. Kwa mfano, katika ubeti wa 15, irabu 'u' imerudiwarudiwa:

Ushikapo utembezi
Ukafuata uzinzi
Fahamu umetuizi
Uso siwezi inua

Mtunzi ametumia takriri irabu ili kuleta wizani na ridhimu katika ushairi wa *Mwana Hasina na Rashidi Walii*.

##### 4.3.3.2 Takriri konsonanti

Takriri konsonanti ni hali ya kurudiwarudiwa konsonanti ile ile katika neno au maneno katika mshororo au ubeti. Kimsingi kurudia huku hutokea mwanzoni lakini inawezekana kupatikana pengine. Muhimu ni kuwa urudiaji huu ujitokeze wazi. Katika ushairi wa Kiswahili takiriri irabu na takiriri konsonanti hazijitokezi sana kama ilivyo katika Kingereza kwani Kiswahili hupendelea muundo wa konsonanti kufuatwa na irabu. Ufuatao ni mfano katika ubeti wa 7:

Kampa kula tamashi
Kwa nguo na dashidashi
Na vikuku kwa makushi
Tena akamuusia

Mtunzi ametumia takriri konsonanti akiwa na nia ya kusisitiza ujumbe wake.

##### 4.3.3.3 Takriri neno

Takriri neno ni urudiaji wa neno ili kuleta msisitizo fulani. Mtunzi amerudiarudia maneno katika matini kwa lengo la kuhimiza. Pamoja na hayo, mtunzi hucheza na maneno ya utungo wenye takiriri ili kuleta mvuto. Aidha, katika ubeti wa 98 anarudia maneno 'Ewe mwana:'

Ewe mwana wa kuzini
Ewe mwana wa maulani
Ewe mwana wa shaitani
Ewe mwana wa udhia

Mtunzi wa *Utenzi wa Mwana Hasina na Rashidi Walii* amefaulu katika matumizi ya mbinu ya takriri. Jambo hili limefanya utenzi huu kuwa wa kuvutia na kunata makini ya wasomaji.

#### 4.3.3.4 Takriri silabi

Takriri silabi ni urudiaji wa silabi za aina moja zinazojitokeza katikati au mwishoni mwa mshororo.Takriri silabi ndio urudiaji ambao hutokea kwa wingi katika tungo za kishairi. Silabi ambazo hurudiwa aghalabu huwa muungano wa konsonanti na vokali. Takriri silabi hutumiwa kama vina vya mishororo ya kila ubeti. Katika *Utenzi wa Mwana Hasina na Rashidi Walii* vina vya mishororo ya kwanza mitatu katika beti nyingi vimerudiwarudiwa. Ufuatao ni mfano katika ubeti wa 193, kina 'na' kimerudiwarudiwa:

Na Yule bibi Hasina
Akuuzwana kunena
Wimbi hii nda kijana
Kwa miarabu unioya

Takriri silabi imesaidia kuleta wizani na pia rithimu katika *Utenzi wa Mwana Hasina na Rashidi Walii.*

### 4.3.4 Chuku

Tulieleza chuku kama tamathali inayotia chumvi kuhusu uwezo wa kiumbe, tabia zao na sifa zao kwa madhumuni ya kusistiza. Mbinu hii pia huitwa udamisi. Mtunzi wa *Utenzi wa Mwana Hasina na Rashidi Walii* ametumia mbinu hii kwa kina. Kwa hivyo, tutatoa mifano michache kutoka kwa utenzi huu. Baadhi ya mifano hii ni kama ifuatayo:

Utashi wa Mwana Hasina umepigiwa chuku. Aidha, mtunzi amemsawiri kama mhusika asiye na maandili. Kwanza, anaenda kinyume na desturi anapomuendea Rashidi na kumpendekezea wawe na uhusiano wa kimapenzi. Pamoja na hayo, Rashidi anapokataa kumtimizia matakwa yake hafi moyo. Badala yake anazindisha juhudi za kumpata. Anabuni mikakati ya kutaka kusoma somo la dini. Aidha, alifanya hivyo kwa vile alijua babake angependekeza Rashidi kuwa mwalimu wake wa dini. Hii ni kwa sababu katika ubeti wa 122, tunajuzwa kuwa mwalimu aliyesifika sana kwa

sababu ya uadilifu wake alikuwa Rashidi. Baada ya mwana Hasina kufaulu kumshawishi babake ampe masomo ya Dini ya Kiislamu, anamwomba amjengee nyumba mbali na mji mahali ambapo hapana kelele, akiwa na lengo la kudumisha ufaragha ili aweze kutimiza lengo lake la kumpata Rashidi. Mtunzi anasema kuwa Rashidi anapokataa kubadili msimamo wake wa awali kuhusu Mwana Hasina, Hasina anajaribu kumshika kwa nguvu ili wazini naye. Juhudi zake zinapogonga mwamba anaenda kwa wachunga mbuzi na kutungwa mimba. Aidha, mtunzi ametia chumvi sifa ya Hasina ya uzinzi kwa vile anataka kuonyesha maudhui ya uasherati.

Pili, kiwango cha utakaso wa Rashidi si cha kawaida. Aidha, mtunzi amemchora kama mhusika mwandilifu kupita kiasi cha ilivyo kwa vijana wa rika lake. Uandilifu wake umepita mipaka. Mtunzi anasema kuwa mhusika huyu hakufanya dhambi yoyote. Pamoja na hayo, alikuwa mhusika mtakatifu. Haya ni katika ubeti wa 25 ambapo tunaelezwa:

Halikufanya maasi
Alimwepua Bilisi
Wala hana majilisi
Pa wenziwe wa kaka

Tatu, mtunzi amepigia chuku kitendo cha Rashidi cha kujikata sehemu nyeti. Mtunzi alitaka kuonyesha maudhui ya uandilifu. Aidha, anatujuza kuwa wakati Rashidi aliombwa na Sultan kuwa mwalimu wa Hasina wa dini, aliomba Sultan muda aende akavikarabati vitabu vyake vya dini. Baadaye tunaambiwa kuwa aliutumia ule muda kwa kuzikata sehemu zake nyeti na kuzikausha. Aidha, baada ya kipindi alichopewa kuisha aliweka nyeti zile kwa mfuko na kumpelekea Sultan. Alimwomba amuhifadhie hirizi ile. Mtunzi amepigia chuku kitendo hiki cha kujikata nyeti kwa vile alitaka kusisitiza kuhusu uandilifu wa Rashidi, na alivyokuwa amesimamia kidete na maamuzi yake ya kutotenda dhambi na liwe liwalo. Tamathali hii imechangia pakubwa katika kumwezesha mtunzi kuwasilisha ujumbe wake. Aidha, imeondoa ukinaifu kwa msomaji na kumpa mshawasha wa kuendelea kusoma kazi husika.

### 4.3.5 Taswira

Taswira ni maneno ambayo hupangwa kisanii katika ushairi ili yaweze kuchora picha kamili ya kitu, hali, wazo, dhana au uzoefu fulani wa jamii au sehemu ya jamii katika mawazo ya wanaopokea ushairi unaohusika. Senkoro (2011), anasema matumizi ya taswira aghalabu huambatana na yale ya ishara ambazo mara nyingi hufichwa ndani ya tamathali za semi. Matumizi mazuri ya taswira na ishara hutegemea ufundi wa mshairi wa kuchota mambo

mbalimbali kutoka katika mazingira yaliyomzunguka yeye na jamii na pia kutoka katika historia na sehemu zingine za maisha azijuazo. Katika *Utenzi wa Mwana Hasina na Rashidi Walii* tutashughulikia aina tatu za taswira. Aina hizi ni: taswira zionekanazo, taswira za mawazo na taswira za hisi.

#### 4.3.5.1 Taswira zionekanazo

Taswira zionekanazo ni aina ya taswira ambayo inaonekana. Aina hii ya taswira imetumika kwa wingi sana katika *Utenzi wa Mwana Hasina na Rashidi Walii*. Katika ubeti wa 30 na 31, Hasina anamtuma Kijakazi amfuate Rashidi ili ajue nyumbani kwake. Pia, baada ya Kijakazi kugundua makazi ya Rashidi, Hasina anamtuma tena ampelekee vitumbua. Kwa hivyo, akilini mwa msomaji taswira kadha zimechoreka, kuanzia ile ya Kijakazi kumfuata Rashidi, Kijakazi akimpelekea Rashidi mchele na pia kumpelekea vitumbua kwa sinia (ubeti wa 34 and 35).

Fauka ya hayo, anatupa picha kamili katika ubeti wa 49, anaeleza kuhusu maandalizi ya Mwana Hasina kabla ya kwenda kwa Rashidi, tunaambiwa kuwa anavalia nguo ya halili. Nguo ya halili ni ishara ya mtu wa tabaka la kifahari. Aidha, katika ubeti wa 51, mtunzi anatupa taswira ya wajihi wa Mwana Hasina. Anatueleza kuwa alikuwa mwanamke wakufanya mvuto kwa watu umbo lake lilikuwa la kuvutia akilinganishwa na wasichana wenzake.

Pia, mbinu hii inadhihirika wakati Rashidi anakata nyeti zake na kuzikausha kisha kuziweka kwa furushi. Hatimaye, anampelekea Sultan na kumwomba amwekee kwa kudai kuwa ilikuwa hirizi. Aidha, wakati Mwana Hasina anamsingizia kuwa alimtunga mimba anamuitisha Sultan hirizi ile. Wanapigwa na butwaa baada ya kuona kuwa Rashidi hakuwa na nyeti zake kwa hivyo haingewezekana kumtunga Hasina mimba.

Fauka ya hayo, malenga anatupa taswira ya yale yaliyotokea wakati Sultani aligundua kuwa Hasina alikuwa mja mzito. Aidha, kwa hamaki anamlazimisha Rashidi kumueleza yaliyojiri. Baadaye Hasina anadai kuwa mimba ilikuwa yake Rashidi. Sultan anamchukua Rashidi na kumweka nguzoni na kuendea fimbo. Aidha, angempiga fimbo mia kama ilivyokuwa sheria.

Pia, mtunzi ametuchorea picha ya yale yaliojiri wakati uongo wa Hasina uridhihirika. Sultan anaagiza mchunga mbuzi aliyemtunga Hasina mimba aletwe. Anapoletwa, anafungwa kwa kamba na kuchapwa fimbo mia akiwa pamoja na Mwana Hasina.

#### 4.3.5.2 Taswira ya mawazo

Taswira ya mawazo ni taswira ambayo ni ya kuwazika. Mtunzi ametumia taswira hii kwa kina. Aidha, kupitia kwa mhusika Rashidi mtunzi anatujuza yale yatakayotokea wakati wa kifo cha mja mwenye dhambi. Tunaelezwa kuwa insi aliye mzinzi atawekwa pingu kwa mikono kisha awekwe mikufu shingoni. Pia, nyoka atatokea na kuukagua uso wake huku akiutemea sumu. Fauku ya hayo, mtunzi anaendelea kusema kuwa mwenye dhambi atalishwa matunda ya zakum na mahali pakuishi patakuwa Jehanamu. Pamoja na hayo, kabla ya mja mwenye dhambi kutolewa roho, malaika watakaokuwa na nari watafika na kumtesa sana. Haya ni katika ubeti 81 – 99.

Hatimaye, tunajuzwa kuwa mwili wa mwenye dhambi utatoa harufu mbaya inayofananishwa na ile ya mfu. Pia, wakati wakuzikwa nyoka yule wa hapo awali atarudi tena na kuukagua uso wake kwa mara ya pili. Mtunzi ametumia taswira hii ya mawazo ili kuonyesha imani ya wafuasi wa Dini na Kiislamu ya jinsi maisha yalivyo baada ya kifo. Taswira hii inamfanya msomaji kuchukia dhambi asije akapatwa na haya baada ya kuaga dunia.

#### 4.3.5.3 Taswira hisia

Taswira hisia ni utumiaji wa maneno fulani yanayoibua hisia fulani akilini mwa msomaji. Aidha, zaweza kuwa hisia chanya au hasi. Hisia hizi huweza kuwa za chuki, furaha, hofu, masikitikiko na kinyaa miongoni mwa nyingine. Ni muhimu kutaja kuwa, taswira hisia huwa na uwezo mkubwa wa kuingia akilini na kupitisha ujumbe kwa hadhira. Aidha, Sultan anapomuomba Rashidi awe mwalimu wa Hasina, sisi kama hadhira tunahofia kuwa Rashidi angenaswa na mtego wa Mwana Hasina. Hii ni kwa sababu ya matukio ya hapo awali ambapo tumeshuhudia juhudi zake Mwana Hasina za kumtongoza Rashidi. Mtunzi ametumia taswira ili kufanya ushairi uwe uhai zaidi. Aidha, ametumia mbinu hii ili kunasa hisia za wasomaji kwa kuwapangia maneno yanayoweza, kuumba picha kamili katika akili zao.

### 4.3.6 Uzungumzinafsia

Uzungumzinafsia ni mbinu ambayo mhusika hujizungumzia. Anaweza kuibua mjadala kuhusu jambo fulani au akarudia maneno ambayo yalizungumzwa na mtu mwingine akiwa peke yake. Mtunzi ametumia mbinu hii kwa kiasi kidogo sana. Katika ubeti wa 62 mtunzi anasema:

Kalala katafakari
Mambo haya ni hatari
Majina ya ifariji
Kenda na jamaa

Maneno katika ubeti huu ni mfano wa uzungumzi nafsia. Kupitia uzungumzaji nafsi, tunapata kujua msimamo wa Rashidi. Aidha, tunaona dhiki iliyomkuba baada yakutembelewa na Hasina.

**4.3.7 Misemo**

Katika sura ya pili tulieleza misemo kama matumizi ya maneno ya kawaida kijozi kwa njia isiyokuwa ya kawaida. Katika *Utenzi wa Mwana Hasina na Rashidi Walii*, mtunzi ametumia misemo kwa kina. Kwa utafiti wetu tumeshughulikia baadhi ya misemo na kudhihirisha ufaafu wake katika utenzi huu.

Katika ubeti wa 109 mshororo wa kwanza, Rashidi amesema, 'Mtenda mema ni mwema' anamwambia Mwana Hasina katika harakati ya kupingana na juhudi zake za kumuadama. Anamuonyesha faida ya kuwa mwema. Aidha, anamjuza kuwa waja wema hawana dosari na ni waandilifu.

Pia, katika ubeti wa 15 mshororo wa kwanza Sultan anasema, 'Ushikapo utembezi'. Msemo huu unamanisha kitendo cha uzinzi. Sultan anatumia msemo huu kumtahadharisha Mwana Hasina dhidi ya kujiingiza kwa uasherati.

Aidha, katika ubeti wa 31, mtunzi anasema:

Kijakazi kenda hima
Kumfuata ghalamu
Hata palipo kuhema
Rashidi akajitia

'Kenda hima' ni msemo. Aidha, malenga anamanisha kuwa Kijakazi alienda mbio alipoenda kupeleleza kuhusu maakazi yake Rashidi.

Mtunzi ametumia misemo kwa lengo la kupamba kazi yake. Pia, ametumia mbinu hii kwa nia ya kusitiri maana na kumfanya msomaji kutafakari ujumbe uliopo.

### 4.3.8 Kinaya

Katika sura ya pili, tulieleza kinaya kama mbinu ya msemaji kutoa kauli ambayo ni kinyume na anachomanisha. Aidha, ni hali ya kutenda kinyume na matarajio ya msomaji. Katika *Utenzi wa Mwana Hasina na Rashidi Walii* mbinu hii imetumika kwa wingi. Aidha, katika utenzi huu kuna aina mbili za kinaya. Kinaya cha hali na kinaya cha kiusemi.

#### 4.3.8.1 Kinaya cha hali

Kinaya cha hali ni pale ambapo matendo ya wahusika yanakuwa kinyume na matarajio ya msomaji. Katika *Utenzi wa Mwana Hasina na Rashidi Walii*, Mwana Hasina ambaye ametokona na aila yenye uwezo mkubwa wa kifedha anamwandama Rashidi ambaye ni masikini na kabila lake lilikuwa duni. Hata hivyo, anashidwa kupata penzi lake.

Pia, Mwana Hasina anaenda kinyume na desturi anapomtongoza Rashidi. Katika jamii ya Kiislamu mwanamke hapaswi kufanya hivyo. Aidha, mwanamume ndiye tu aliye na idhini ya kumpembeja mwanamke. Pamoja na hayo, Mwana Hasina anapokataliwa na Rashidi, anaenda kwa wachunga mbuzi. Anazini na mmoja wao na kutungwa mimba. Kama tulivyotaja hapo awali ametokana na aila tajiri kwa hivyo ni kinaya kuona jinsi alivyoichusha hadhi yake.

#### 4.3.8.2 Kinaya cha kiusemi

Kinaya cha kiusemi ni pale ambapo usemi fulani una maana iliyo kinyume. Katika *Utenzi wa Mwana Hasina na Rashidi Walii*, mtunzi anatujuza katika ubeti wa 23 – 24 kuwa, mhusika Rashidi hakufanya dhambi tangu kuzaliwa. Katika ubeti wa 69 tunaelekezwa kuwa, huenda kila mara kutubu dhambi zake. Mtunzi ametumia kinaya kuonyesha kinyume cha matarajio au mwonoulimwengu wa jamii kuhusiana na jinsi ambavyo mtoto wa kike anavyopaswa kujimudu. Pia, ametumia kinaya kuashiria kuwa ni nadra sana kwa binadamu kuwa mwongofu kiasi cha kutotenda dhambi yoyote tangu kuzaliwa.

### 4.3.9 Uhuishi

Katika sura ya pili, tulieleza uhuishi kama tamathali ambayo inavipa vitu visivyo na uhai au sifa walizonazo binadamu sifa za kibinadamu. Aidha, sifa hizi za uhai hulenga kuvitukuza vitu hivyo. Katika *Utenzi wa Mwana Hasina na Rashidi Walii*, mtunzi ametumia mbinu hii ingawa kwa

kiasi kidogo. Katika ubeti wa 94, mtunzi anasema kuwa wakati mwili wa mja mwenye dhambi utawekwa kwa jeneza, nyoka atafika na kuukagua uso wake huku akisema:

Atasema kwa lizani
Ewe mwana wa kuzini
Ghururi ya duniani
Iliyoko kuhadaa

Katika ubeti huu nyoka amepewa uwezo wa kuukagua uso wa insi mwenye dhambi ambao ni uwezo wa kibinadamu.

Pia, katika ubeti wa 98, nyoka huyu amepewa uwezo wa kuzungumza. Katika ubeti huo, mtunzi anasema ifuatayo:

Ewe mwana wa kusini
Ewe mwana maluuni
Ewe mwana shaitani
Ewe mwana wa udhia

Aidha, katika ubeti wa 95 mtunzi anasema ‘Ghururi ya dunia’. Hapa ulimwengu umepewa sifa za uhai kwa vile tujuavyo kuwa, kitu kilicho na uhai ndicho huwa na uwezo huu wa kuwa na kiburi. Mtunzi ametumia mbinu hii kwa kusudi la kuipa uhai kazi yake. Hii inasaidia msomaji kujihusisha na hisia za mtunzi moja kwa moja na kujiweka mahali pake.

### 4.3.10 Methali

Tulieleza methali kama semi fupi zinazoeleza mawazo au mafunzo ambayo ni mazito na hutokana na uzoefu wa jamii. Katika *Utenzi wa Mwana Hasina na Rashidi Walii* mtunzi ametumia methali moja tu. Aidha, ametumia methali ‘mchimba kisima huingia mwenyewe’ katika ubeti wa 97. Methali inamrejelea Mwana Hasina ambaye alinuia kumuangamiza Rashidi baada ya kukataa kuzini naye. Hatimaye, mpango wake unagonga mwamba na anaishia kwa maangamizi. Mtunzi ametumia methali hii kututahadharisha dhidi ya kujihusisha na matendo yatakayodhuru wengine, kwa vile matendo yale yaweza kuishia kutuhini sisi.

### 4.3.11 Nidaa

Katika sura ya pili, tulieleza kuwa mtunzi hutumia alama za hisi katika kuonyesha mshangao au msistizo. Mbinu hii ya kutumia alama ya hisi ndio hufahamika kama nidaa au usiyahi. Mbinu hii imetumika kwa uchache sana. Aidha, katika ubeti wa 98 mtunzi anasema:

Ewe mwana wa kuzini!
Ewe mwana wa maluuni!
Ewe mwana wa shaitani!
Ewe mwana wa udhia!

Mtunzi ametumia mbinu hii katika kujenga hisia za hasira katika huo ubeti. Pia, jambo hili limesaidia msomaji kujihusisha na hisia za mtunzi moja kwa moja.

### 4.3.12 Istiari

Tulieleza istiari kama mbinu ya kulinganisha kitu na kingine bila kutumia vihusishi vilinganishi. Katika *Utenzi wa Mwana Hasina na Rashidi Walii*, ubeti wa 174, Mwana Hasina anasema 'kumbe si mtu ni nyama' Mwana Hasina anamfananisha Rashidi na mnyama kwa kudai kuwa kitendo cha utungishaji mimba ndiye aliyemtendea. Mbinu hii imechangia kuchora taswira ya kimawazo inayomfanya msomaji kuwelewa zaidi anachokizangumzia.

## 4.4 Usimulizi

Katika sura ya pili, tulieleza usimulizi kama jinsi matukio yanavyosimuliwa katika kazi ya kifasihi. Aidha, msimulizi huweza kuchukua mitindo ya aina tatu ikiwemo nafsi ya kwanza, ya pili na ya tatu.

*Utenzi wa Mwana Hasina na Rashidi Walii* unaelekea kuchanganya nafsi ya kwanza na usimulizi maizi. Kulingana na Wamitila (2008), usimulizi maizi huhusishwa na nafsi ya tatu. Msimulizi huanza kusimulia kwa nafsi ya kwanza ambayo hupotea hadi mwishoni. Huu ndio usimulizi unaodhihirika pakubwa katika *Utenzi wa Mwana Hasina na Rashidi Walii*. Msimulizi ameanza kwa nafsi ya kwanza katika beti za kwanza nne ambapo anamshukuru Mwenyezi Mungu, Muhammad na aila yake. Aidha, katika ubeti wa nne anatujuza kuwa anataka kusimulia hadithi. Katika beti hizi nne ametumia kiambishi 'ni' ambacho ni kiwakilishi cha nafsi ya kwanza umoja. Ufuatao ni mfano wa ubeti wa 4:

Nimeona hadithi katiti
Sultan mwenye nti
Kavya wake binti
Kijani yeye mmoya

Vivyo hivyo katika beti za mwisho, ambapo mtunzi anarejelea nafsi ya kwanza na kutujuza kuwa amehitimisha usimulizi wake. Kisha anasema jina lake ni Saidi na jina la babake ni Abdala. Ufuatao ni mfano wa ubeti wa 201:

Nimetunga tenzi nyingi
Nimesema mambo mangi
Nikisema watu wangi
Nadhani watatukiwa

Mtunzi ametumia kiwakilishi cha nafsi ya kwanza ‘ni’.

Zaidi ya hayo, baada ya kujitambulisha ambapo tumesema kuwa mtunzi ametumia nafsi ya kwanza, mtunzi amebadili mkondo wa usimuliaji ambapo amehusisha nafsi ya tatu. Aidha, anasimulia hadithi kuhusu Sultan aliyekuwa na mwana wa kipekee aliyeitwa Mwana Hasina. Ametumia kiwakilishi cha nafsi ya tatu katika kusimulia kisa hiki. Haya ni katika ubeti wa 5, hadi ubeti wa 199.

Hata hivyo, mtunzi anawajumuisha wahusika wake mara kwa mara. Aidha, anawapa nafasi ya kutoa maoni, kwa mfano, katika ubeti wa 15, Sultan anamwelezea Mwana Hasina wasiwasi wake kumhusu, ambapo anasema:

Ushikapo utembezi
Ukuafuata uzinzi
Fahamu umetuizi
Uso usiweli kuinua

Katika kutoa haya maoni, Sultan anatumia kiwakilishi cha nafsi ya pili ‘u’

Usimulizi huu unampa mhusika nafasi ya kushiriki katika utenzi na kuleta uhai. Aidha, mhusika anapotoa mawazo yake anaeleweka zaidi na hadhira kuliko kama angekuwa anasimuliwa na mtu mwingine.

Matumizi ya nafsi ya tatu katika *Utenzi wa Mwana Hasina na Rashidi Walii* umempa msimulizi nafasi ya kutathmni na kutoa maoni mbalimbali. Aidha, katika ubeti wa 24 msimulizi anaeleza sifa za Rashidi anaposema hakufanya dhambi na alimhepa Ibilisi. Pia, katika ubeti wa 25 anazidi kueleza sifa hizi, anasema alikuwa kijana mtanashati na mtakatifu. Fauku ya hayo, hakuwahi fanya maovu. Msimulizi anatathmini haya akiwa nje ya hadithi. Mtindo wa nafsi mseto umemfanya mtunzi kufaulu katika kuwasilisha ujumbe wake.

### 4.5 Hitimisho

Katika sura ya nne, tumehakiki kipengele cha mtindo ambapo tumeshughulikia matumizi ya lugha na usimulizi. Tumebaini kuwa *Utenzi wa Mwana Hasina na Rashidi Walii* umetumia mbinu za uhuru wa kishairi wa aina mbalimbali, vilevile utenzi huu una matumizi ya tamathali za semi kwa wingi. Tamathali za usemi zenye zimetumika kwa kina ni taswira na takriri miongoni mwa zingine. Kwa upande mwingine tumebainisha kuwa mtunzi ametumia nafsi mseto katika kusimulia *Utenzi wa Mwana Hasina na Rashidi Walii*.

## SURA YA TANO

## TATHIMINI NA MAPENDEKEZO

### 5.1 Utangulizi

Katika sura hii tumejadili kwa kifupi muhtasari na matokeo ya utafiti wetu. Aidha, matokeo haya ndiyo yatakayotuwezesha kupima nadharia tete tulizozitaja hapo mwanzoni na malengo yetu. Fauku ya hayo, tunatoa mapendekezo ya utafiti zaidi.

### 5.2 Muhtasari wa utafiti

Katika utafiti wetu, tuliazimia kubainisha vipengele vya fani katika *Utenzi wa Mwana Hasina na Rashidi Walii* na jinsi vilivyotumika katika kuwasilisha ujumbe wa mtunzi kwa hadhira. Aidha, tuliazimia kuangalia jinsi mtunzi alivyotumia fani mbalimbali na kuwasilisha ujumbe wake kwa hadhira. Tumeigawa tasnifu katika sura tano.

Sura ya kwanza ilihusu utangulizi wa utafiti wetu. Katika sehemu hii tulieleza maswala ya utangulizi au ya kimsingi ya utafiti wetu. Masuala haya ni pamoja na mada ya utafiti, tatizo la utafiti, sababu za kuchagua mada, nadharia tete, malengo ya utafiti, yaliyoandikwa kuhusu mada na njia za utafiti.

Katika sura ya pili, tumetaja na kutoa fasili vipengele mbalimbali vya kifani. Aidha, tumetolea mifano ya kijumla ya vipengele vya kifani tulivyovitaja. Vipengele hivi ni: Muundo, mandhari, msuko, matumizi ya lugha na wahusika na uhusika huku tukijikita kwa mifano kutoka kwa tenzi zingine. Katika sura ya tatu, tumehakiki: Msuko, muundo mandhari na wahusika na uhusika kwa kujikita katika *Utenzi wa Mwana Hasina na Rashidi Walii*. Tumeona kuwa *Utenzi wa Mwana Hasina na Rashidi Walii* una muundo sahili. Aidha, muundo wa utenzi umefuata kaida za utunzi wa tenzi. Fauka ya hayo, tumehakiki kipengele cha mandhari ambapo utenzi huu una mseto wa mandhari. Kwa mfano: Mandhari ya kiwakati, kidhahania na dini. Zaidi ya hayo, tumeshughulikia wahusika ambapo tumebainisha kuwa kuna wahusika mbalimbali kama vile: Wajenzi, wakuu na wasaidizi miongoni mwa wengine.

Katika sura ya nne, tumehakiki matumizi ya lugha katika *Utenzi wa Mwana Hasina na Rashidi Walii*. Vipengele tulivyoshughulikia ni uhuru wa kishairi na tamathali za semi. Aidha, tumeona kuwa mtunzi ametumia uhuru wa kishairi na tamathali za usemi kwa ufundi mkubwa. Pia,

matumizi ya lugha yana mchango mkubwa katika kufanikisha uwasilishaji wa ujumbe, mandhari na kusawiri wahusika. Fauka ya hayo, tumeshughulikia usimulizi wa *Utenzi wa Mwana Hasina na Rashidi Walii.*

Tumetabua kuwa *Utenzi wa Mwana Hasina na Rashidi Walii* umejengeka kwa misingi ya fani. Aidha, tumethibitisha matumizi ya Kingozi, Kiamu na pia msamiati wa Kiarabu labda sababu ikiwa ndiyo msingi wa dini ya Kiislamu. Matumizi ya lahaja yamechangia pakubwa sana utajiri wa msamiati katika utenzi huu. Pamoja na hayo, mwandishi ameonyesha waledi wake wa kutumia tamathali kadhaa za usemi ili kuwasilisha ujumbe. Haya matumizi yamechangia sana kumvutia msomaji.

### 5.3 Kuhusu malengo ya utafiti

Katika utafiti huu, tulitaka kubainisha vipengele vya fani katika *Utenzi wa Mwana Hasina na Rashidi Walii*. Tuliweza kuafiki madhumuni haya katika sura ya tatu. Tumehakiki na tumebainisha kuwa msuko wa utendi huu ni sahili kwa vile unatiririka kutoka mwanzo hadi mwisho na hakuna urejeshi. Muundo katika utenzi huu umefuata kaida mbalimbali kama zinavyoelezwa na wataalamu mbalimbali wa fasihi ya Kiswahili. Aidha, tumegundua kuwa katika *Utenzi wa Mwana Hasina na Rashidi Walii* una mandhari mseto kama vile, Uswahilini, Kidhahania na Dini miongoni mwa nyingine. Tumetambua kuwa wahusika katika *Utenzi wa Mwana Hasina na Rashidi Walii* ni wa aina mbalimbali. Kuna wahusika wakuu, wa mraba mmoja, wahusika wasaidizi na wahusika wajenzi.

Katika sura ya nne, tumehakiki matumizi ya lugha. Katika matumizi ya lugha, tumezungumzia kuhusu matumizi ya uhuru wa kishairi na matumizi ya tamathali za usemi. Tumeona kuwa mtunzi ametumia uhuru mbalimbali wa kishairi kama vile: Mazida, tabdila, inkisari na uhuru wa kisintaksia. Pia, mtunzi ametumia misamiati ya Kingozi na vilevile Kiamu na baadhi ya msamiati wa Kiarabu. Mtunzi ametumia tamathali za semi kwa wingi. Tamathali tulizoziangalia ni pamoja na tashbihi, takriri, nidaa, chuku, kinaya, misemo, takriri na tashbiha ambazo zimedhirika sana katika *Utenzi wa Mwana Hasina na Rashidi* Walii. Aidha, tumeshughulikia usimulizi japo kwa kifupi tu.

Kwa ujumla, madhumuni ya kubainisha fani iliyotumiwa na mtunzi yalitekelezwa katika sura ya tatu na ya nne.

Madhumuni ya pili yalikuwa kuhakiki mchango wa vipengele vya fani katika *Utenzi wa Mwana Hasina na Rashidi Walii*. Tumebaini kuwa vipengele vya fani vina mchango mkubwa sana katika kuwasilisha maana na dhamira ya utendi huu. Maana imebainika kutokana na fani mbalimbali. Hali kadhalika, vipashio vya fani vimesaidia kuleta taswira kamili ya hali ya mambo. Bila ya vipengele hivi vya fani, maana ya utenzi huu na taswira zake hazingejitokeza kikamilifu na kwa uwazi. Aidha, fani imesaidia katika kuupa *Utenzi wa Mwana Hasina na Rashidi Walii* uzuri na mvuto wa kuvutia hadhira. Zaidi ya hayo, fani ina mchango mkubwa sana katika *Utenzi wa Mwana Hasina na Rashidi Walii*.

### 5.4 Utathmini wa nadharia tete

Nadharia tete ya kwanza ilisema kwamba, vipengele vya fani katika *Utenzi wa Mwana Hasina na Rashidi Walii* ndivyo nguzo kuu iliyotumika katika ujenzi wa utenzi wenyewe. Hii imethibitika kupitia jinsi vipengele vya fani vinavyoibuka kuwa mhimili wa kazi yote ya utunzi ambapo pasingekuwa na kipengele hiki, mtunzi hangefanikiwa kuwasilisha ujumbe wake. Vipengele vya fani ambavyo ni nguzo kuu ni kama vile: Msuko, muundo, mandhari, wahusika na uhusika na mtindo.

Nadharia tete ya pili ya utafiti huu ilisema kwamba, fani katika *Utenzi wa Mwana Hasina na Rashidi Walii* imechangia kuwasilisha maana katika utendi wenyewe. Tumethibitisha nadharia hii kuwa ya ukweli. Kutokana na matumizi ya lugha, msimulizi ameweza kuwasilisha maana ya aliyoshamiria katika utenzi huu. Tamathali za usemi anazozitumia zimechangia katika kuibua masuala muhimu ambayo mtunzi alilenga kuwasilisha katika kazi yake. Aidha, matumizi yake ya lugha kwa njia ya kiufundi imechangia sana katika kutupa taswira ya mandhari. Pamoja na hayo, fani imechangia kwa kiasi kikubwa katika ujenzi wa wahusika katika *Utenzi wa Mwana Hasina na Rashidi Walii*. Pia, matukio yamepangwa kwa njia ya moja kwa moja na kwa hivyo kusaidia katika kutiririsha maana na kuifanya kuwa rahisi kueleweka.

Kwa muhtasari, *Mtunzi wa Utenzi wa Mwana Hasina na Rashidi Walii* amefaulu katika utunzi wake. Aidha, mtunzi amefanya usimulizi wake vizuri. Fauku ya hayo, amefanya hivyo kwa kusawiri wahusika mbalimbali. Pia, ametumia msuko sahili ambao unasaidia kueleweka kwa utenzi huu kwa njia rahisi. Fani ya *Utenzi wa Mwana Hasina na Rashidi Walii* imeingiliana vizuri na ni vingumu kutenganisha vipengele vyake mbalimbali.

### 5.5 Mapendekezo

Tumehakiki fani katika *Utenzi wa Mwana Hasina na Rashidi Walii*. Aidha, kama tulivyotaja katika sababu ya kuchagua mada, *Utenzi wa Mwana Hasina na Rashidi Walii* haujawahi kufanyiwa uhakiki wa kiusomi. Ulihaririwa na kutafsiriwa na Jan Knappert. Kwa hivyo, tungependekeza watafiti wengine washughulikia kipengele cha maudhui na dhamira ya utenzi huu. Fani pia inaweza kuhakikiwa kwa kutumia nadharia tofauti na Urasimu wa Kirusi. Pamoja na hayo, ulinganishi unaweza kufanya baina ya utenzi huu na tenzi zingine za Kiswahili kuhusu fani. Aidha, usawiri wa mwanamke pia waweza kushughulikiwa katika utenzi huu.

## MAREJELEO


Abedi, K.A. (1954). *Sheria za Kutunga Mashairi na Diwani ya Amri*. Nairobi: KLB.

Beckson, K. / Granz, A.(1996). *A Reader guide to Literary Terms*. London: Themes and Hudson.

Buchbinder, D. (1991). *Contemporary Literary Theory and the Reading of Poetry*. Moray: Macmillan Education Astralia, PTY.

Eartich, V. (1969). *Russian Formalism*, 3rd Edition. The Hague: Mouton and C.o.N.V. Publishers.

Fokkema, D. & Ibsch, E. (1978). *Theory of Literature in the Twentieth Century*. London: Hurst and Co. Ltd.

Gill, R. (1985). *Mastering English Literature*. London: The Macmillan Press Ltd.

Habwe, J. / Karanja, P. (2007). *Misingi ya Sarufi ya Kiswahili*. Nairobi: Phoenix Publishers.

Ibrahim, N.S. (1988). *Tungo Zetu na Msingi wa Mashairi na Tungo Nyingine*. Trenton: The Red Sea Press Inc.

Karanja, M. (2014). "Matumizi ya Istilahi na Tashbiha katika Diwani ya *Sauti ya Dhiki*". Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Nairobi. Haijachapishwa

Kisilu, P.N. (2003). "Mwingiliano wa Fani na Maudhui katika *Ushairi wa Kithaka wa Mberia*". Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Nairobi. Haijachapishwa.

Kitula, K. / Amata, J. (2001). *Taaluma ya Ushairi*. Nairobi: Acacia Stante.

Knappert, J. (1979). *Four Centuries of Swahili Verse. A literary History and Anthology*. London: Heinemann Educational Book Ltd.

Kuhenga, C. (1997). *Tamathali za Usemi*. Dar es Salaam: East Africa Literature Bureau.

Lugwiri, P.L. (2011). "Istiari, Tashbiha na Taashira katika *Utenzi wa Tambuka*". Tasnifu ya Uzamili ambayo haijachapishwa. Chuo Kikuu cha Nairobi.

Mbatiah, M. (2001). *Kamusi ya Fasihi*. Nairobi : Standard Textbooks Graphics and Publishing.

Mgullu, R.S. (1999). *Mtalaa wa Isimu*: *Fonetiki, Fonolojia na Mofolojia ya Kiswahili*. Nairobi; Longhorn Publishers (K) Ltd.

Mishra, K. (2011). *A Study of Form and Content. Journal of English and Literature*. India; I.S.S.N Publishers.

Mohammad, S.A. (1995). *Kunga za Nathari ya Kiswahili. Riwaya, Tamthilia na Hadithi Fupi*. Nairobi. East African Educational Publishers.

Mugenda, O. & Mugenda, A.G. (1999). *Research Methods*: *Quantitative and Qualitative Approches*. Nairobi: Act Press.

Mwangangi, F.M.(1996). "Uhakiki wa Fani katika Tamthilia Nne za Kitsao". *Uasi* (1980), *Malimwengu Ulimwengu* (1987), *Tazama Mbele* (1987) na *Bibi Arusi* (1983). Tasnifu ya Uzamili ambayo haijachapishwa. Chuo Kikuu cha Nairobi.

Mwangi, I. / Wamalwa, K. (2016). *Miali ya Ushairi: Shule za Upili na Vyuo Vya Elimu*. Nairobi. East African Educational Publishers.

Mwilaria, R. (2011). "Fani katika Utenzi wa Ayub". Tasnifu ya Uzamili ambayo haijachapishwa. Chuo Kikuu cha Nairobi.

Ngara, E. (1985). *Art and ideology in the African Novel; A study of the influence of Marxism on African Writing*. Nairobi: Heinemann.

Njogu, K. / Chemerah, R. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi. Nadharia na Mbinu*. Nairobi: K.L.B

Njogu, K. / Wafula, R.M. (2007). *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Omwayo, O. (1997). "Fani katika Ushairi wa Hassan Mwalimu Mbega: Uhakiki wa *Upisho wa Malenga na Dafina ya Malenga*". Tasnifu ya Uzamili ambayo haijachapishwa. Chuo Kikuu cha Nairobi.

Senkoro, F.E (2011). *Fasihi: Mfululizo wa Lugha na Fasihi Kitabu cha Kwanza*. Dar es Salaam. Kauttis Ltd.

TUKI, (1981). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Nairobi: Oxford.

Wa Mutiso, K. (1996). "Archaetypl Motifs in Swahili Islamic: *Kasida ya Burudai*". Tasnifu ya Shahada ya Uzamifu: Chuo Kikuu cha Nairobi. Haijachapishwa.

Walleck, R. / Warren, A.(1949). *Theory of Literature*. Hansworth: Penguin Books Ltd.

Wamitila, K.W. (2002). *Uhakiki wa Fasihi. Misingi na Vipengele Vyake*. Nairobi : Phoenix Publishers.

Wamitila, K.W. (2003). *Kamusi ya Fasihi na Istilahi na Nadharia*. Nairobi: Focus Publishers.

Wamitila, K.W. (2008). *Kanzi ya Fasihi*: *Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*. Nairobi: Vudemuwa Publishers Ltd.

Wesa, R. (2005). "Uhakiki wa Kifani Katika *Utenzi wa Mwana Fatuma*". Tasnifu ya Uzamili ambayo haijachapishwa. Chuo Kikuu cha Nairobi.